# Ripoti za Nchi Kuhusu Mwenendo wa Haki za Binadamu – 2007

Imetolewa na Ofisi ya Demokrasia, Haki za Binadamu na Kazi ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani

Machi 11, 2008

## Dibaji

Kama Rais Bush alivyosema, "Uhuru unaweza kuzuiwa, na uhuru unaweza kucheleweshwa, lakini uhuru hauwezi kukataliwa." Hatimae, raia wanaojitoa kwa ajili ya kutetea utu na haki watashinda, kama vile kina Havel na Mandela walivyofanya kabla yao. Kama watu hao mashuhuri, watetezi wengi wa leo wa haki za binadamu wanashutumiwa, waliteswa na kukashifiwa kama wasaliti, na kukandamizwa na serikali zao wenyewe – kwa sababu tu ya kung'ang'ania uhuru uliotajwa kwenye Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu, la Umoja wa Mataifa. Wazalendo hawa waliokosa subira ni mfano kwa wananchi wenzao, na kiwango cha juu walichoonyesha kinaendelea kuwapa watu matumaini mahali popote wanaofanya kazi kwa amani kwa ajili ya uhuru wao, utu na haki zao.

Maadili haya ni vipaji vya msingi vya binadamu wote, na njia ya uhakika ya kuvilinda na kuvihifadhi kupitia utawala unaofaa, wa kisheria na kidemokrasia. Uhakika ni kwamba, hakuna njia ya taifa lolote kuelekea demokrasia ambayo ni rahisi na iliyonyooka. Njiani, kuna kujikwaa na vizuizi. Hata kuwepo na mazingira bora, si rahisi kubadili maadili ya kidemokrasia kuwa asasi nzuri za kidemokrasia. Mpito kuelekea demokrasia unaweza kuwa katika mazingira magumu, na maendeleo yanaweza kushindwa kwa sababu ya kukosa uimara na usalama; kupambana na ujinga na maradhi. Serikali zilizojaa rushwa au zisizo na raslimali za kutosha zinaweza kushindwa kufikia matumaini makubwa ya watu wao, hivyo kuwafanya wapoteze imani katika ahadi yao ya maisha bora. Viongozi ambao hawajajitoa vya kutosha kwenye mabadiliko wanaweza kugeukia katika tabia za kimabavu au kuchukua njia zisizofaa kutoka katika utawala wa sheria. Serikali nyingine hazijachukua hata hatua ya kwanza kuelekea kuwahakikishia raia haki zao.

Changamoto hizi kwa haki za binadamu, na nyingine nyingi, zimerekodiwa kikamilifu kwenye rekodi ifuatayo ya nchi. Waraka huu bado unakusanywa na kuandikwa kwa kuamini kuwa hakuna pembe yoyote ya dunia hii ambayo itadumu katika udhalimu. Mabadiliko yanaweza yakachukua muda, lakini mabadiliko yatakuja. Kwa kuwa wananchi duniani kote wanapigania maadili ya haki za binadamu kwa wote, kuna matumaini kuwa, na tunaendelea kuamini kuwa ni jukumu la serikali husika popote pale kuwaunga mkono wanaume na wanawake hawa majasiri.

Kwa moyo huo, ninawasilisha <u>*Ripoti za Nchi kuhusu Mwenendo wa Haki za Binadamu za 2007*</u> za Wizara ya Mambo ya Nje kwa Bunge la Marekani.

Condoleezza Rice
*Waziri wa Mambo ya Nje*

## Maelezo ya Jumla

### Kwa nini Ripoti Zinatayarishwa

Ripoti hii inawasilishwa Bungeni na Wizara ya Mambo ya Nje kulingana na Sehemu ya 116 (d) na 502 B (b) ya Sheria ya Msaada kutoka Nje ya 1961 (FAA), kama ilivyorekebishwa. Sheria inamruhusu Waziri wa Mambo ya Nje kuwasilisha kwa Spika wa Bunge la Wawakilishi na Kamati ya Uhusiano wa Kimataifa ya Seneti ifikapo Februari 25 "ripoti kamili" inayohusu hali ya haki za binadamu zinazotambuliwa kimataifa, ndani ya maana ya kifungu kidogo (A) kwa nchi ambazo zinapokea msaada chini ya sehemu hii, na (B) katika nchi nyingine zote za nje ambazo ni wanachama wa Umoja wa Mataifa na ambazo vinginevyo hazihusiki kwenye ripoti ya haki za binadamu chini ya Sheria hii." Tumeingiza pia ripoti ya baadhi ya nchi ambazo hazimo kwenye makundi yaliyoanzishwa na sheria hizi na kwamba hazimo kwenye masharti ya kibunge.

Mwanzoni mwa miaka ya 1970 Marekani ilirasimisha jukumu lake la kuzungumza kwa niaba ya Viwango vya Kimataifa vya Haki za Binadamu. Mwaka 1976 Bunge lilitunga Sheria ya kuanzisha Mratibu wa Haki za Binadamu katika Wizara ya Mambo ya Nje; nafasi ambayo baadae ilipandishwa na kuwa Naibu Waziri. Mwaka 1994 Bunge lilianzisha cheo cha Mshauri Mwandamizi wa Haki za Wanawake. Aidha Bunge liliandika kuwa sheria masharti rasmi ambayo sera ya nje na biashara ya Marekani inazingatia haki za binadamu za nchi na utekelezaji wa haki za wafanyakazi na kwamba ripoti za nchi ziwasilishwe Bungeni kila mwaka. Ripoti ya kwanza, mwaka 1977, ilijumuisha nchi 82 tu zinazopata msaada wa Marekani;mwaka huu ripoti 196 zinawasilishwa.

### Jinsi Ripoti Zinavyotayarishwa

Mwaka 1993 Waziri wa Mambo ya Nje aliimarisha jitihada za haki za binadamu za balozi zetu kwa kuzitaka sehemu zote kuchangia taarifa na kuthibitisha ripoti za ukiukaji wa haki za binadamu, na kulikuwa na juhudi mpya za kuunganisha mipango ya kazi maalumu kwa ajili ya kuendeleza haki za binadamu na demokrasia. Mwaka 1994 Wizara ya Mambo ya Nje ilipanga upya Ofisi ya Haki za Binadamu na Masuala ya Kibinadamu, na kuiita Ofisi ya Demokrasia, Haki za Binadamu na Kazi. Hatua hii iliakisi mwendo wa nguvu na mkabala uliolenga zaidi masuala yanayounganisha haki za binadamu, haki za wafanyakazi na demokrasia. Kama sehemu ya jitihada hizo, Ripoti ya Mwaka ya Nchi kuhusu utekelezaji wa Haki za Binadamu inawakilisha jitihada zinazoendelea za ofisi za kuripoti ukiukaji wa haki za binadamu. Ripoti inaakisi kazi iliyofanywa na mamia ya wafanyakazi wa Wizara ya Mambo ya Nje, Ofisi za Ubalozi; na wengine wa Serikali ya Marekani.

Balozi zetu, ambazo zilitayarisha rasimu ya awali ya ripoti, zilikusanya taarifa kwa mwaka mzima kutoka vyanzo mbalimbali katika spektra za kisiasa, zikijumuisha viongozi wa serikali; wanasheria, vyanzo vya majeshi yenye silaha, waandishi wa habari, wafuatiliaji wa haki za binadamu, wasomi, na wanaharakati wa kazi. Ukusanyaji wa taarifa unaweza kuwa wa hatari, na maofisa wa Ofisi za Ubalozi wa Marekani mara

nyingi wanakwenda ndani zaidi, kujaribu na wakati mwingine katika mazingira ya hatari; kuchunguza ripoti za udhalilishaji wa haki za binadamu, kufuatilia uchaguzi, na kuwasaidia watu walio hatarini; kama vile wapinzani wa kisiasa na watetezi wa haki za binadamu ambao haki zao zinatishiwa na serikali zao.

Baada ya balozi mbalimbali kukamilisha rasimu zao, zilitumwa Washington kwa aili ya kupitiwa na Ofisi ya Demokrasia, Haki za Binadamu na Kazi; kwa kushirikiana na ofisi nyingine za Wizara ya Mambo ya Nje. Walipokuwa wakifanya kazi kuthibitisha, kuchambua, na kuzihariri ripoti; Maofisa wa Wizara walitumia vyanzo vyao vya taarifa. Hizi zilijumuisha ripoti zilizotolewa na Mareakani na vikundi vingine vya haki za binadamu, viongozi wa nje wa serikali; wawakilishi kutoka Umoja wa Mataifa na Mashirika na asasi nyingine za Kimataifa na kikanda, wataalamu kutoka akademia, na vyombo vya habari. Aidha Maofisa walishauriana na wataalamu kuhusu haki za wafanyakazi; masuala ya wakimbizi, mada za jeshi na polisi, masuala ya wanawake, na masuala ya Sheria. Kanuni iliyoongoza ilikuwa kuhakikisha kuwa taarifa zote zilitathminiwa bila upendeleo, kwa makini, na kwa haki.

Ripoti zilizomo kwenye juzuu hii zitatumiwa kama raslimali za kurekebisha sera, kuendesha diplomasia, na kutoa msaada, mafunzo, na migao mingine ya raslimali. Aidha zitatumika kama msingi wa ushirikiano wa Serikali ya Marekani na vikundi binafsi ili kuendeleza uzingativu wa haki za binadamu zinazotambuliwa Kimataifa.

Ripoti za Nchi za Mwenendo wa Haki za Binadamu zinahusisha watu wanaotambuliwa kimataifa, haki za raia, za kisiasa na za wafanyakazi, kama zilivyotangazwa kwenye Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu. Haki hizi zinajumuisha kutokuteswa au ukatili mwingine, vitendo visivyo vya kibinadamu au vya kudhalilisha au adhabu, kuwekwa kizuizini kwa muda mrefu bila kufunguliwa mashtaka, kutoweka au kuwekwa kizuizini kwa siri; na ukiukaji wa dhahiri wa haki ya kuishi, uhuru na usalama wa mtu.

Haki za Binadamu kwa wote zina lengo la kuingiza heshima kwa utu wa mtu katika michakato ya serikali na sheria. Watu wote wana haki ya kubadilisha serikali yao kwa njia ya amani na kunufaika na uhuru wa msingi; kama vile uhuru wa kusema, kujiunga na chama, kukusanyika, kutembea, na dini, bila ya ubaguzi wa kimbari, dini, asili ya utaifa, au jinsi. Haki ya kujiunga na chama huru cha wafanyakazi ni sharti la lazima kwa jamii na uchumi huru. Kwa hiyo ripoti zinatathmini haki za msingi za mfanyakazi zinazotambuliwa kimataifa, zikijumuisha haki ya kujiunga na chama, haki ya kujiunga na kujadili kwa pamoja, ukatazaji wa kazi za kushurutishwa au kulazimishwa, hali ya ajira ya mtoto, kiwango cha umri wa chini wa ajira ya mtoto, na masharti ya kazi yanayokubalika.

**Utangulizi**

Kuheshimu haki za binadamu na uhuru wa msingi ulioakisiwa kwenye Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu, ni kama Rais Bush alivyosema kuwa, msingi wa uhuru, haki na amani katika dunia." Hivi leo, katika kila bara, wanaume na wanawake wanafanya kazi, mara nyingi dhidi ya tofauti na hatari kubwa, kupata haki za msingi ili kuishi kwa heshima, kufuata fahamu zao na kutoa mawazo yao bila hofu, kuwachagua wanaotaka kuwaongoza na kuwajibisha viongozi wao, na kupata haki sawa chini ya Sheria.

Kuongezeka kwa demokrasia kunaonekana kama aina ya serikali inayoweza kupata haki hizo na uhuru wa msingi. Hakuna aina ya serikali ambayo haina dosari. Demokrasia ni mfumo wa serikali ya watu, na kwa ajili ya watu, inayozingatia kanuni inayosema kwamba binadamu ana haki ya asili ya kurekebisha mustakabali wao wenyewe, lakini kwamba ni viumbe vyenye dosari na kwamba lazima vijengwe katika marekebisho. Wananchi wetu wanataja historia ya fahari ya mapambano katika kila kizazi kwa kuwa taifa letu linaweka msingi wa kuleta taratibu za kidemokrasia karibu na kanuni zetu zinazohifadhiwa kwa upendo mkubwa, hasa tukiwa tunataka kukabiliana na udhalimu na changamoto za kila zama mpya.

Tunapochapisha ripoti hizi, Wizara ya Mambo ya Nje inabaki ikizingatia mambo yanayokosolewa ya kimataifa na kitaifa ya rekodi za haki za binadamu za Marekani. Serikali ya Marekani itaendelea kusikiliza na kujibu kwa uwazi wasiwasi wowote kuhusu taratibu zetu, ikiwa ni pamoja na hatua ambazo tumechukua kulinda taifa letu dhidi ya tishio la ugaidi duniani. Sheria, sera na taratibu zimebadilika sana katika miaka ya hivi karibuni; na tunaendelea kujitahidi kulinda raia wasio na hatia na uhuru wa msingi. Kama sehemu ya juhudi hizi, Marekani inawasilisha ripoti kwa vyombo vya Kimataifa kulingana na wajibu wake chini ya mikataba mbalimbali ya haki za binadamu ambayo ni mshiriki.

Tunazingatia kwa makini ahadi zetu zote na, kwa juhudi zetu za nia njema kutimiza ahadi hizo, tunathamini dhima muhimu inayofanywa na vyama vya kiraia na vyombo huru vya habari.

Hatuangalii maoni kuhusu utendaji wetu yanayotolewa na wengine katika jumuiya ya kimataifa katika kuingilia masuala yetu ya ndani; wala serikali nyingine kuangalia mawazo kuhusu utendaji wao kikwelikweli. Hakika, chini ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu, ni sahihi na ni jukumu la kila mtu na kila chombo cha jamii kuendeleza heshima kwa ajili ya haki hizi na uhuru na kwa hatua za kimaendeleo, kitaifa na kimataifa, ili kupata utambuzi na uzingativu wao kwa wote na unaofaa.

Ripoti hizi zilizoagizwa na bunge zinaelezea utendaji katika mwaka 2007 za mashirika mengine duniani katika kutekeleza ahadi za kimataifa kuhusu haki za binadamu. Ripoti zitaifahamisha serikali ya Marekani inayotunga sera na pia zitakuwa kama marejeo kwa serikali nyingine, asasi za serikali mbalimbali; asasi zisizo za kiserikali, watu binafsi na vyombo vya habari. Kila ripoti ya nchi inajizungumzia yenyewe. Baadhi ya maoni

mtambuko yanaweza, hata hivyo kuchukuliwa kutoka kwenye ripoti zinazohusu maendeleo ya haki za binadamu na kanuni za demokrasia duniani kote. Mifano mahususi ya nchi tunayotoa hapa chini inamaanisha kuwa kielelezo, si ya kukamilisha kabisa.

Jitihada za Marekani za kuendeleza haki za binadamu na uhuru wa kidemokrasia duniani kote zinaakisi maadili makuu ya wananchi wa Marekani. Aidha wanaendeleza maslahi yetu muhimu. Kama Rais Bush alivyosema: "Uhuru si haki ya kujadiliwa ya kila mwanamume, mwanamke, na mtoto, na njia ya kuelekea kwenye amani ya kudumu katika dunia ni uhuru."

Tunaunganisha maadili na maslahi yetu tunapofanya kazi kwa ushirikiano na watetezi wenzetu wa demokrasia na haki za binadamu na kujenga mfumo wa kidemokrasia katika kufichua udhalilishaji na kuendeleza uvumilivu, kulinda haki za kimaadili na za waumini wachache na wafanyakazi kuendeleza haki sawa za wanawake na kusitisha biashara ya watu. Maadili na maslahi yetu kamwe hayawezi kwenda pamoja pale tunaposaidia maendeleo, vyama huru vya kiraia, kuhakikisha kuwepo na uchaguzi huru na wa haki na kuimarisha demokrasia inayozingatia sheria. Kila mara watetezi wa haki za binadamu wanapoathiriwa na uonevu, maadili yetu ya muda mrefu na maslahi yetu yanalindwa tunapoonyesha kwa maneno na vitendo mshikamano wetu unaotuunganisha nao.

**Tanzania**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye idadi ya watu ya takriban milioni 39.3, ni jamhuri inayofuata mfumo wa vyama vingi inayojumuisha bara na fungu. Visiwa vya Zanzibar. Muungano unaongozwa na rais, ambaye pia ni mkuu wa serikali, na chombo kimoja cha kutunga sheria ambacho ni Bunge. Pamoja na kwamba, Zanzibar imeunganishwa kwenye mfumo wa serikali na chama wa nchi, ina rais wake, mfumo wa mahakama, na baraza la kutunga sheria, na inaendelea kufanya mambo yake kwa uhuru. Kwenye uchaguzi wa mwaka 2005 wa rais na wabunge, Jakaya Kikwete alichaguliwa kuwa rais, na chama tawala Chama cha Mapinduzi (CCM) kilikuwa na viti vingi bungeni. Waangalizi waliuona uchaguzi wa muungano katika pande zote mbili za bara na Zanzibar kuwa ulikuwa huru na haki kabisa. Hata hivyo, uchaguzi wa 2005 wa rais kwa upande wa Zanzibar ulikuwa na ubishani, wenye dosari kubwa na vurugu zilizochochewa kisiasa. wakati mamlaka za kiraia kwa ujumla zilidhibiti majeshi ya usalama, kulikuwa na matukio kadhaa ambapo askari wa majeshi ya usalama walifanya kazi peke yake bila ya mamlaka za Serikali.

Kulikuwa na matukio kadhaa yaliyoendelea ya matatizo ya haki za binadamu. Polisi na walinzi wa magereza walitumia nguvu kubwa dhidi ya wafungwa au watuhumiwa, na wakati mwingine kufikia kusababisha kifo, na suala la polisi kutochukuliwa hatua limebaki kuwa ni tatizo; kulikuwa na taarifa zilizoendelea za mauaji ya wazee waliotuhumiwa kuwa wachawi; mazingira ya magereza yalikuwa mabaya na ya kutishia maisha; rushwa ilienea kwa kiasi kikubwa miongoni mwa polisi na uvunjaji wa taratibu za kisheria; idara ya mahakama ilikabiliwa na rushwa na kukosa ufanisi, hususani katika mahakama za mwanzo; uhuru wa kuzungumza na uhuru wa vyombo vya habari ulikuwa mdogo; rushwa ilienea serikalini; mamlaka zilizuia kutembea kwa wakimbizi; vurugu katika jamii dhidi ya wanawake zilizidi; na biashara ya watu na ajira ya watoto yalikuwa ni matatizo.

**KUHESHIMU HAKI ZA BINADAMU**
**Sehemu ya 1: Kuheshimu Utu wa mtu, Ikiwa ni Pamoja na Uhuru wa:**

**a. Kutotwaliwa maisha isivyo halali au Kiholela**

Hakukuwepo na mauaji yaliyochochewa kisiasa na serikali au maofisa wake wa usalama katika mwaka; hata hivyo mara kadhaa majeshi ya usalama yalitumia nguvu kubwa iliyosababisha mauaji ya raia, wakiwemo watu waliokuwa kizuizini.

Katika mwaka huo maofisa waandamizi wa polisi waliwatuhumu maofisa wa polisi wa ngazi za chini kwa mauaji ya watu kadhaa kinyume na sheria. Kwa mfano, mnamo Januari maofisa wa polisi; Fanuel John, Emil Said, na Yona Fika walikamatwa kwa mauaji ya watu wawili akiwemo mwanafunzi wa shule ya msingi katika wilaya ya Tarime ya Mkoa wa Mara wakati wa kuwakamata wanakijiji waliokuwa wakiuza bangi na pombe haramu. Mkuu wa Mkoa Isidori Shirima aliunda kamati ya watu watano ya kuchunguza tukio hilo.

Uchunguzi ulikuwa ukisubiri uamuzi hadi mwishoni mwa mwaka. Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Habari la Reuters, mnamo Septemba 7 polisi mkoani Kilimanjaro waliwaua watuhumiwa 14 wa ujambazi kwa kuwavamia, 11 miongoni mwao walibainishwa kuwa ni Wakenya, akiwemo mwanamke. Hadi mwishoni mwa mwaka uchunguzi ulikuwa unaendelea. Kwa mujibu wa Reuters, kundi la wanaharakati wa haki za binadamu wa Kenya walikwenda Tanznaia kuchunguza tukio hilo; waliwekwa kizuizini na baadae wakaachiwa baada ya Ubalozi wa Kenya kuingilia kati.

Katika mwaka huo mamlaka ziliwafungulia mashtaka maofisa polisi waliohusika katika kuwafyatulia risasi na kuwaua wafanyabiashara wa madini watatu na dereva wa teksi karibu na Dar es Salaam Januari 2006. Tume maalumu iliyoongozwa na jaji wa mahakama kuu ilichunguza tukio na kugundua kuwa waathirika hawakuwa majambazi kama polisi walivyodai, na iliripotiwa kuwa hawakukataa kukamatwa. Hadi mwisho wa mwaka kesi ilikuwa bado ikisubiri uamuzi.

Vifo vilivyotokana na ghasia za kundi la watu wenye hasira viliendelea, ikiwa ni pamoja na kutupiwa mawe, kupigwa, kukatwakatwa na mapanga na kuchomwa moto, lakini walikuwa ni wachache kufuatia kampeni ya serikali ya kupiga vita ghasia za makundi ya watu wenye hasira. Kwa mujibu wa gazeti la Citizen la tarehe 24 Januari, Tumaini Mesiaki aliuwawa na kundi la watu akijaribu kuiba kwenye nyumba. Marehemu alikuwa miongoni mwa wafungwa waliopewa msamaha na Rais Kikwete mwaka 2006. Mnamo Machi 6, gazeti la The Guardian lilitoa picha za mwizi aliyepigwa mawe hadi kufa na watu waliokuwa na hasira. Daily News la Julai 8 liliripoti kupigwa hadi kufa Duka Selemani wa Wilaya ya Mbeya baada ya kuiba madebe mawili ya kahawa kutoka kwa mwanakijiji mwingine. Mashtaka katika kesi hizo yalikuwa nadra, mamlaka zilieleza kuwa mashahidi walisita kutoa ushahidi.

Mauaji ya watuhumiwa wa uchawi yaliendelea. Imani iliyoenea ya uchawi ilisababisha kuuawa kwa watu wengi waliotuhumiwa kuwa ni wachawi na watu waliodai kuwa ni waathirika wao, pia ndugu wenye hasira wa waathirika, au watu wenye ghasia. Utaratibu huu ambao ulifanyika zaidi mkoani Shinyanga, ulienea katika mikoa mingine kutokana na wachungaji waliokuwa wakihama kutoka Shinyanga. Kwa mfano, kwa mujibu wa gazeti la Majira la Februari 14, watu wasiofahamika walimchoma kisu hadi kufa Atuhalile Kiswaga mwenye umri wa miaka 65 katika mkoa wa Iringa. Kulingana na Habari Leo la Julai 21, watu wasiofahamika walimuua Kundi Kusinza mwenye umri wa miaka 60 mkoani Mwanza kwa kutumia mapanga na kuchukua viungo vya siri vya marehemu. Mkoani Mwanza polisi walitoa taarifa ya kifo cha mwanamke kilichohusishwa na uchawi na walikuwa wanachunguza tukio.

Mnamo Agosti 2006 gazeti la The African, likitaja takwimu kutoka Asasi isiyo ya Serikali (AISE) Concern for the Elderly (COEL), liliripoti kuwa, katika muongo uliopita wazee 8,580 katika eneo la Ziwa waliuawa kufuatia tuhuma za uchawi. COEL ilionyesha kuwa matukio ya namna hii hutokea pia katika mikoa ya Tabora, Mwanza, Shinyanga, na Kigoma.

Serikali iliwafungulia mashtaka watu waliotuhumiwa kuwaua watu waliodhaniwa kuwa wachawi, lakini mashitaka yalikuwa magumu kwa kuwa wahusika wa mauaji wamejifunza kukwepa mamlaka za sheria.

Iliripotiwa Desemba kuwa miezi mitatu ya mwanzo maalbino wanne waliuawa, huenda ni kwa sababu ya imani za kuwa viungo vyao vya mwili vingetumiwa kuwapa watu utajiri. Hadi mwisho wa mwaka hakuna watu waliokamatwa; Chama cha Maalbino Tanzania kilionyesha wasiwasi wao kwa serikali kwa kupuuzia mauaji haya.

**b. Utowekaji**

Hapakuwa na ripoti za utowekaji uliochochewa kisiasa

**c. Utesaji na Vitendo vya kikatili vya kinyama au Udhalilishwaji au Adhabu**

Katiba na Sheria vinazuia vitendo kama hivyo visifanyike. Hata hivyo, ripoti ziliendelea kuwepo kwamba polisi waliwatesa watu, kuwatishia na vinginevyo kuwatendea vibaya wahalifu waliotuhumiwa na wafungwa katika mwaka huo; Vipigo na viboko vilikuwa ndizo njia zilizotumika sana. Kwa mujibu wa ripoti za vyombo vya habari, ni idadi ndogo sana ya polisi ndiyo iliyopatikana na hatia kwa kuwadhalilisha wafungwa katika mwaka huo, kufuatia kushitakiwa kwa mara kwa mara kwa polisi wahalifu.

Viongozi wa Serikali za Mitaa mara chache walitumia viboko kama adhabu kwa watoto wahalifu na watu wazima, na walimu na viongozi wa shule walitumia viboko na aina nyingine ya dhabu za kutandika wanafunzi viboko. Kwa mfano, mnamo Julai 30 Daily News liliripoti kuwa Richard Dimond mwenye umri wa miaka 28 na James Malango mwenye umri wa miaka 21 walihukumiwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Sumbawanga kwenda jela miaka 126 na viboko 20 kwa wizi wa kutumia silaha na ubakaji. Utumiaji wa viboko uliendelea kupungua shuleni katika mwaka huo, kufuatia juhudi za Wizara ya Elimu na vyombo vya Habari, lakini uliendelea kutumika kwenye hukumu za jinai.

Kulikuwa na ripoti chache zaidi katika mwaka huo za wanajeshi waliowapiga raia; Hata hivyo, mwezi Mei; Shirika la Human Right Watch (HRW) liliripoti kuwa majeshi ya usalama yaliwadhalilisha Wanyarwanda na Warundi ambao walikuwa wakifukuzwa nchini. Kwa mujibu wa maelezo ya HRW, wanajeshi, polisi na wanamgambo wa Tanzania waliwapiga na kuwatishia watu waliokuwa wakiwafukuza, huku wakiwapora na kuharibu mali zao. Katika matukio mengine wazazi walitenganishwa na watoto wao wakiwemo watoto wachanga. Polisi pia walishutumiwa kwa kupokonya na kuharibu nyaraka ambazo zingethibitisha kuwa baadhi ya watu waliolengwa walikuwa watu walioandikishwa uraia wa Tanzania. HRW lilidai kuwa serikali ilishindwa kutoa tahadhari ya kutosha ya kuwaondoa kwa Serikali za Rwanda na Burundi au kwa mashirika ya kibinadamu, na kwamba wengi wa hao waliofukuzwa walipata matatizo ya upungufu wa chakula, kuni, na makazi.

Katika mwaka huo kulikuwepo na ripoti za polisi kudhalilisha watu kingono walio kizuizini bara na Zanzibar.

**Hali katika Magereza na Vituo vya Mahabusu**

Hali ya magereza iliendelea kuwa ya kikatili na ya kutishia maisha. Magonjwa yalikuwa ni kitu cha kawaida na yalisababisha vifo vingi magerezani. Kulingana na ripoti za AZISE, vyanzo vya vifo vilivyoongoza vilikuwa Malaria, kifua kikuu, VVU/UKIMWI, kipindupindu, na magonjwa mengine yaliyohusiana na uchafu. Zahanati za magereza zilitoa matibabu kwa kiwango kidogo tu, na marafiki na wanafamilia wa wafungwa kwa kawaida walipaswa kupeleka dawa au fedha za kununulia dawa hizo. Mwezi Februari, katika kuzuia kuenea kwa VVU/UKIMWI magerezani, serikali ilianzisha vituo 12 vya unasihi na upimaji wa hiari ili kutoa huduma kwa asasi za kutoa adhabu.

Zaidi ya magonjwa ya kuambukiza, serikali ilikiri kuwepo kwa matatizo makubwa ya msongamano wa watu, mahabusu kuwekwa kizuizini kwa muda mrefu, na kuwachanganya magerezani watoto na watu wazima. Mwaka 2006 magereza ya humu nchini yalikuwa na wafungwa waliohukumiwa 23,968 na waliowekwa kizuizini wakisubiri hukumu 21,017 hivyo kufanya jumla ya wafungwa 44,985, ambapo uwezo wa mwisho wa huduma za magereza za humu nchini ni wafungwa 23,000.

Wafungwa walikabiliwa na mazingira mabaya ya kuishi na walikosa huduma za msingi. AZISE ziliripoti kuwa wafungwa walipewa chakula kibaya kutokana na viwango vya chini sana vya afya na usafi.

Kulikuwa na ripoti za walinzi kuwapiga na kuwadhalilisha kingono wafungwa katika mwaka huo. Kwa mfano, Februari 25, polisi huko bara walimkamata Koplo Onesphory Materu kwa kumbaka msichana mfungwa mwenye umri wa miaka 15. Huko Zanzibar, kulingana na gazeti la Guardian la Agosti 15, askari polisi mmoja alisimamishwa kazi kwa kumbaka msichana wa shule kwenye kituo cha polisi ambako alikwenda kuripoti kuwa alikuwa amebakwa na mtu. Kaimu Kamanda wa Polisi wa Unguja ya Kusini; Khamis Ramadhan, aliwaambia waandishi wa habari kuwa polisi walikuwa wakichunguza tukio hilo na walikuwa wakisubiri ripoti ya daktari kabla ya kuchukua hatua zaidi za kisheria dhidi ya askari huyo. Hadi mwisho wa mwaka uchunguzi wa matukio yote mawili ulikuwa ukisubiri uamuzi.

Mnamo Januari 17, Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Kisutu ilianza kusikiliza kesi ya 2005 ambayo walinzi wa magereza tisa walishtakiwa kwa kuwashambulia na kuwajeruhi waandishi wa habari wawili; kulingana na Daily News. Hadi mwisho wa mwaka kesi ilikuwa bado inasubiri uamuzi.

Machi 27 gazeti la This Day liliripoti kuwa baada ya mgomo wa gereza, walinzi waliwahoji wafungwa na kuwalazimisha kukubali tuhuma za uongo. Wafungwa walidai pia kwamba walitishwa na kugofywa na maofisa waandamizi wa polisi.

Agosti 14 gazeti la Dar Leo liliripoti kuwa viongozi wa magereza waliwapiga vikali na kuwaweka kizuizini vijana wanane baada ya kiongozi wa gereza kuwatuhumu baadhi yao kwa kumwibia. Vijana walidai kuwa viongozi hao walichukua fedha na simu zao za mikononi.

Hakukuwa na maendeleo zaidi katika kesi ya 2005 dhidi ya kiongozi wa gereza aliyetuhumiwa kuwadhalilisha wanamgambo wawili waliokuwa mahabusu.

Sheria inataka wafungwa watenganishwe kwa kuzingatia umri na jenda; hata hivyo, katika hali halisi magereza mengi yenye msongamano hayakuwa na vyumba maalum vya wafungwa wanaume, wanawake na watoto wadogo. Mwaka 2006 kulikuwa na takriban magereza 10 maalum kwa wafungwa watoto katika nchi nzima, lakini kwa sababu ya msongamano, wafungwa wenye umri wa miaka kati ya 18 na 21 walifungwa kwenye jela za watu wazima. Kwa hali hiyo magereza yalitakiwa kuwatenganisha watoto na wafungwa watu wazima nyakati za usiku. Mnamo Machi 25, Daily News lilimnukuu Hakimu Mkuu Mkazi wa Mahakama ya watoto bara, Hamisa Kalombola, akisema kuwa nchi ilikuwa na shule moja tu iliyoidhinishwa ya wahalifu watoto na nyumba 5 za rumande au jela ya watoto. Alisema kuwa upungufu wa magereza na uhaba wa maofisa wa uangalizi ulilazimisha mahakama kuwaweka watoto waliohukumiwa chini ya uangalizi na kutozwa faini au kuachiwa kwa masharti badala ya kufungwa jela. Gazeti lilimnukuu Ofisa uangalizi akisema kuwa ukosefu wa sehemu ya wasichana katika jela pekee mkoani Mbeya umelazimisha mahakama kutoa hukumu mbadala kwa wasichana.

Mara nyingi Mamlaka zilihamisha wafungwa kwenda magereza mbalimbali bila ya kuwaarifu ndugu na familia za wafungwa.

Mnamo Februari 14 gazeti la Majira liliripoti kuwa wafungwa wanne waliopatikana na hatia ya kuua walikataa kupanda kwenye basi ili wapelekwe gereza la Ruanda mkoani Mbeya kwa sababu hawakupewa nakala ya hukumu ambayo walihitaji kwa ajili ya kukata rufaa. Mgomo ulidumu kwa dakika 30 kabla ya polisi kutumia nguvu ya kuwalazimisha wafungwa kuingia kwenye basi.

Mnamo Machi 12, zaidi ya wafungwa 12 walisusia kusikilizwa kwa kesi katika mahakama ya Dar es salaam kupinga kuachiwa kwa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Ditopile Mzuzuri, ambaye alipewa dhamana baada ya waendesha mashtaka kupunguza uzito wa shtaka kutoka uuaji na kuwa uuaji bila kukusudia miezi mitatu baada ya kukamatwa. Wafungwa nchini kote walifanya mgomo, wakiishutumu mahakama kwa kutoa upendeleo kwa Mzuzuri na wafungwa wengine wanaofahamika na kuwapuuza wale ambao wamekuwa wakisubiri kusikilizwa kwa maombi yao ya dhamana kwa karibu miaka 10. Baadae ripoti za magazeti zilisema kuwa wafungwa walioongoza mgomo Dar es salaam walihojiwa na kutishwa na viongozi wa gereza. Mnamo Machi 29, wafungwa wanane katika Gereza la Mtwara walikataa kuingia chumba cha mahakama na kila mmoja alifungwa kwa mwaka mmoja. Migomo hii ilimfanya Waziri wa Mambo ya Ndani, Joseph Mungai, kuwaonya maofisa magereza kwenye Mkutano wa Siku Mbili wa

mwezi Mei wa Maofisa Waandamizi wa Magereza mjini Dar es Salaam dhidi ya vitendo vibaya wanavyofanyiwa wafungwa wakiwa wanatumikia vifungo vyao.

AZISE za hapa nchini, Mashirika ya Kimataifa na watazamaji wa kidiplomasia waliruhusiwa kufuatilia hali ya magereza katika mwaka huu. Mwezi Mei Chama cha Msalaba Mwekundu kilitembelea Gereza la Segerea hapa Dar es Salaam. Kamati ya Kimataifa ya Chama cha Msalaba Mwekundu iliwatembelea wafungwa katika Mahakama ya Kimataifa ya Mauaji ya Rwanda, jijini Arusha. Ofisi ya Wakimbizi ya Umoja wa Mataifa (UNHCR) ilitembelea magereza yenye wakimbizi kuona hali yao ya uhamiaji na kutoa msaada kwa wale wanaoamini kuwa walikamatwa kinyume cha sheria na kuhukumiwa kwa uhamiaji haramu. AZISE za Kimataifa na za kitaifa pia ziliwatembelea wafungwa na kuwapa msaada wa kisheria na kibinadamu.

Katika mwaka huo, Kamisheni ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya bara, chombo huru kilichoteuliwa na serikali, ilitembelea idadi kubwa ya magereza ya wanaume, ya wanawake na ya watoto kukagua hali ya wafungwa pamoja na chakulan a maji, huduma za vyoo, msongamano katika vyumba vya kulala. Aidha Kamisheni ilikagua hali ya maisha ya walinzi na mfumo wa kuhifadhi chakula. Wafungwa walilalamika kwa kamisheni. Kuhusu kukaa kwa muda mrefu kizuizini, kutokuwa na nakala za uamuzi au hukumu wanazozihitaji kwa ajili ya kukata rufaa, kuwekwa karibu sana na wafungwa wanaougua kifua kikuu, kukosa mablanketi, na kufanyiwa uchunguzi wa miili yao wanapoingia na wanapotoka magerezani. Kisheria Kamisheni lazima iwasilishe ripoti serikalini; Idara ya Magereza na kisha kuyapanga magereza katika madaraja. Ripoti na madaraja viwe wazi kwa ajili ya wananchi kuzisoma.

**d. Ukamataji wa Watu Kiholela au kuwatia Kizuizini**

Katiba inakataza ukamataji wa watu kiholela na kuwatia kizuizini; hata hivyo mambo haya mawili yalikuwa ni matatizo. Kwa mfano, mnamo Februari 3 gazeti la This Day liliripoti kuwa baadhi ya askari polisi huko Arusha waliwapokonya watu pesa kwa kuwatishia kuwakamata kwa mashtaka ya uongo ya kukutwa na dawa za kulevya. Katika makala, kamanda wa polisi wa mkoa wa Arusha, Basilio Matei alithibitisha kuwa ofisa mrakibu/mfawidhi alikuwa akiwachunguza askari polisi wanne na kundi la wanamgambo kwa kuomba fedha kwa nguvu au simu za mkononi kutoka kwa wakazi wa Arusha.

Mnamo Julai 22 toleo la Habari Leo, wakazi wa eneo la Tunduma katika wilaya ya Mbozi mkoani Mbeya walilalamika kwa Kamanda wa Polisi ya Mkoa, Suleiman Kova, kuhusu askari polisi waliowabughudhi kwa kuwaomba hongo. Wakazi hao walidai kuwa wale ambao walishindwa kulipa walikamatwa kwa mashtaka ya uongo.

**Dhima ya Polisi na Vyombo vya Usalama**

Jeshi la Polisi la Taifa, chini ya Wizara ya Usalama wa Raia ina wajibu wa kwanza wa kudumisha sheria na utulivu. Kikosi cha Jeshi la Kuzuia Ghasia ni sehemu ya Jeshi la Polisi. Walinzi wa sungusungu, wanaofanya kazi pamoja na viongozi wa Serikali za Mitaa, vilisaidia Jeshi la Polisi, ikiwa ni pamoja na katika kambi za wakimbizi. Kitengo

kimoja cha Wizara ya Ulinzi kinahusika na Usalama wa Nje na majukumu mengine ya usalama wa ndani. Jeshi la polisi linaendelea kupewa fedha pungufu na kukosa ufanisi.

Polisi hutumia nguvu kubwa, rushwa ndani ya polisi, na kinga yalikuwa ni matatizo makubwa. Kwa mfano, toleo la Julai 22 la Habari Leo lilichapisha malalamiko ya wanavijiji wa Mkoa wa Mbeya kwa Kamanda wa polisi wa mkoa kuhusu maofisa walio chini ya kikosi chake ambao waliwaweka wenyeji kizuizini mara kwa mara kwa makosa ambayo hawakufanya na kuwaomba hongo kabla ya kuwaachia.

Mara nyingi raia walilalamika kuwa polisi walichelewesha kupeleleza uhalifu na kuwafungulia mashtaka wahalifu. Kwa mfano, Januari 13, toleo la The Guardian liliripoti kuwa kiongozi mmoja wa Serikali ya Mtaa mwakilishi wa Kata ya Vikumburu aliwashutumu polisi wa wilaya ya Kisarawe kwa kuwalinda watu waliowapa mimba wasichana wa shule. Alisema kuwa hakuna hatua zilizochukuliwa dhidi ya wahalifu pamoja na kuwepo na malalamiko ya wazazi na walezi.

Ingawaje wanasheria na polisi hawakufanya kazi kama waendesha mashtaka wa serikali katika mahakama za mwanzo, wataalamu wengi wa mambo ya mahakama walikosoa utaratibu huu, ambao ulishutumiwa kuwaruhusu polisi kutengeneza ushahidi katika kesi za jinai. Kwa mujibu wa ripoti ya AISE, kuna wakati polisi walikosa ushahidi, na watuhumiwa walifanikiwa kukwepa mashtaka kwa kuwahonga maofisa wa polisi. Polisi pia walitumia vitisho vya ukamataji watu kiholela ili kuwapokonya pesa. Jamii inaona kuna upungufu mkubwa wa ulinzi katikati ya ongezeko la uhalifu unaofanywa na watu wenye silaha. Toleo la Juni la gazeti la Uhuru linalomilikiwa na serikali liliripoti kuwa Mkurugenzi wa Uendeshaji Mashtaka wa Serikali, Eliezer Feleshi; aliagiza Waendesha Mashtaka kufanya kazi zao kwa kufuata utawala wa sheria na si kwa maslahi ya wakubwa wao.

Katika mwaka huo kulikuwa na matukio kadhaa ya watu wenye hasira waliojichukulia sheria mkononi. Mnamo Desemba 20, Daily News liliripoti tukio ambalo watu watatu waliteswa na kuuawa wakati watu waliokuwa na hasira walipowachoma moto kwa ajili ya kufanya uvuvi haramu.

Aidha gazeti hilohilo lilichapisha makala iliyoelezea jinsi watu waliokuwa na hasira walivyomuua mtu aliyeiba kuku wawili. Mara nyingi Watuhumiwa walitoa pesa na kutoka mahabusu; wananchi pamoja na vyombo vya habari viliwalaumu polisi na mahakama kwa kutokuchukua hatua zinazofaa na hivyo kuchukua "Sheria za mtaani" dhidi ya wahalifu.

Kuliendelea kuwepo na ripoti za vyombo vya habari pamoja na malalamiko kutoka kwenye vikundi vya vyama vya kiraia na wananchi kuhusu rushwa miongoni mwa polisi katika mwaka huo. Kwa mfano, Mamlaka ya Mapato Tanzania mkoa wa Mbeya ilikamata gari mali ya Kikosi cha Polisi wa Kuzuia Ghasia lililokuwa limebeba tani moja ya sukari ya magendo kutoka mpakani mwa Tanzania na Malawi kwenda Dar es salaam. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya alisema kuwa halitambui gari hilo kwa sababu halikuwa la mkoani kwake. Taasisi ya Kuzuia na kupambana na Rushwa, chombo cha

kupambana na rushwa nchini; iliripoti malalamiko mengi ya wananchi ya rushwa ambayo yalihusisha Jeshi la Polisi na mamlaka za mitaa. Novemba 2006 vyombo vya habari viliripoti kuwa dawa za kulevya zilizokuwa na thamani ya maelfu ya dola ziliibwa zikiwa chini ya ulinzi wa polisi katika Kikosi cha Kupambana na Dawa za Kulevya kilichoko Dar es Salaam. Kamanda wa Kikosi alibadilishwa, na askari wawili walikamatwa. Hadi mwisho wa mwaka kesi ilikuwa bado inasubiri uamuzi, kwa kuwa ni mashahidi wawili tu wa upande wa uendeshaji mashtaka ndio walitoa ushahidi.

Mnamo Januari 2006 Rais Kikwete aliiagiza Wizara ya Usalama wa Raia na maofisa waandamizi wa polisi kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya ofisa yeyote ambaye anakiuka maadili. Mnamo Machi 2006, Jeshi la Polisi lilianza kumchunguza sajenti wa polisi aliyetuhumiwa kumiliki mali isiyolingana na kipato chake. Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalumu ya Dar es Salaam Alfred Tibaigana alieleza kuwa ofisa huyo akikutwa na makosa atafukuzwa kazi. Katika mwaka huohuo Tibaigana alisema pia kwamba ofisa mwingine aliyetuhumiwa kushirikiana na raia kuiba mali kwenye nyumba pia akikutwa na hatia atafukuzwa kazi. Hadi mwisho wa mwaka uchunguzi ulikuwa unasubiri uamuzi.

Zipo taratibu za ndani kwenye jeshi la polisi za kuchunguza tuhuma za udhalilishaji unaofanywa na polisi; pamoja na mabadiliko, tabia ya polisi inayoendelea inamaanisha kwamba hazijatumika ipasavyo.

Katika mwaka huo jeshi la polisi liliendesha semina za mafunzo kuhusu upelelezi, haki za binadamu, kuharakisha uchunguzi, kumaliza kesi za jinai, na kuwashughulikia wanachama au viongozi wa vyama vya upinzani. Mara kadhaa, polisi walishirikiana na wataalamu wa mafunzo wa Kimataifa. Mwezi Mei, polisi 43, viongozi wa mahakama, na viongozi wa uhamiaji walimaliza kozi ya majuma mawili kuhusu mbinu za uchunguzi wa jinai katika kesi za biashara ya watu.

Sheria inatoa hadhi ya kisheria kwa vikundi vya jirani na vijiji vya Sungusungu vinavyopambana na uhalifu. Serikali za Mitaa ziliwateua watu kwa msaada wa kaya mojamoja ambazo ziliamua ni nani miongoni mwao angejiunga na ulinzi wa sungusungu. Sungusungu wameendelea kujizatiti katika maeneo ya vijijini na kwenye kambi za wakimbizi, lakini hawakuwepo katika maeneo mengi ya mijini. Sungusungu wana mamlaka ya kuwakamata watu, lakini hawabebi silaha/bunduki isipokuwa rungu kwa ajili ya ulinzi. Sungusungu wameshutumiwa kwa kutumia nguvu zaidi, ikiwa ni pamoja na kuwapiga watuhumiwa, wakati mwingine hata kusababisha kifo. Kwa mfano mnamo Mei 28 The Guardian liliripoti kuwa mabishano baina ya polisi na kundi la wanafunzi wa shule ya sekondari, waliokuwa na hasira kutokana na kukamatwa wenzao wawili waliokutwa na gramu 0.5 ya bangi, yaligeuka vurugu wakati sungusungu 10 walipofika kuwasaidia polisi. Kwa mujibu wa gazeti hilo, wanafunzi waliwazidi polisi nguvu na sungusungu wakapiga yowe. Wanakijiji waliokuwa na silaha waliwasaidia polisi na sungusungu; vurugu/ghasia zilisababisha kifo cha mwanafunzi mmoja na wengine watano kujeruhiwa. Ilikuwa ni desturi ya wakazi wa jirani na sungusungu wanapolinda ama kuwachangia kiasi kidogo cha fedha kwaajili ya ulinzi au kutoa mtu mmoja kutoka kwenye kaya zao kushiriki kwenye ulinzi. Katika kambi za wakimbizi, zaidi ya kikosi

cha polisi cha mara kwa mara, vikundi vya sungusungu vilivyojumuisha wakimbizi vilifanya shughuli zao kwa kiasi fulani kama jeshi la usalama.

**Kukamatwa na Kuwekwa kizuizini**

Sheria inataka watu watiwe mbarano kwa hati kwa kuzingatia ushahidi wa kutosha, na mamlaka kulingana na sheria. Aidha sheria inamtaka mtu anayekamatwa kwa uhalifu, tofauti na mahabusu wa usalama wa taifa, ashtakiwe mbele ya mahakama ndani ya saa 24 baada ya kukamatwa; hata hivyo, kiutendaji polisi walishindwa kutekeleza sharti hili. Sheria inawapa watuhumiwa haki ya kuwasiliana na mwanasheria au kuzungumza na wanafamilia, lakini wakati mwingine mamlaka iliwanyima haki hii. Kupata ushauri wa haraka kumekuwa kugumu kutokana na ukosefu wa wanasheria katika maeneo ya vijijini, ukosefu wa mawasiliAno na miundombinu, na kutokujua kusoma na kuandika na umaskini wa watuhumiwa. Mamlaka ziliwapa haraka mahabusu taarifa ya mashtaka dhidi yao. Serikali ilitoa uwakilishi wa kisheria kwa washtakiwa fukara na kwa watuhumiwa wote walioshtakiwa kwa mauaji au uhaini. Sheria hairuhusu uwezekano wa dhamana kwa makosa ya mauaji na uhaini. Kulingana na hukumu ya mahakama kuu ya Julai 13, jopo la majaji watatu mjini Dar es salaam linadhani kukatalia dhamana kwa kosa la wizi wa kutumia silaha si kikatiba na iliipa serikali miezi 18 ya kufanya mabadiliko muhimu ya sheria. Wakati dhamana inatolewa kwa baadhi ya kesi, masharti makali kuhusu uhuru wa kutembea na kukutana yanawekwa. Katika mahakama za mwanzo na za wilaya, wakati mwingine rushwa ndiyo iliamua dhamana itolewe au isitolewe.

Chini ya Sheria ya kuwekwa kizuizini, rais anaweza kuamuru kukamatwa na kuwekwa kizuizini kwa muda usiofahamika kwa mtu yeyote anayedhaniwa kuwa ni hatari kwa amani ya wananchi au usalama wa taifa. Sheria inataka kwamba serikali iwaachie watu waliowekwa kizuizini chini ya sheria hii ndani ya siku 15 tangu kuwekwa kizuizini au kuwataarifu sababu za kuwekwa kizuizini; aidha inamruhusu mahabusu aliyewekwa kizuizini kuhoji misingi ya kuwekwa kwake kizuizini katika vipindi vya siku 90. Serikali ina uwezo mkubwa wa kumweka mtu kizuizini chini ya sheria, ambao unawaruhusu wakuu wa mikoa na wilaya kuwakamata na kuwaweka kizuizini ndani ya saa 48 watu ambao wanaweza "kuharibu utulivu wa raia." Sheria hii haikutumika katika mwaka huo.

Mnamo Julai 2006, Waziri wa Sheria na Masuala ya Katiba Mary Nagu alisema kuwa mahakama za sheria zilipokea maombi 36 yanayohusiana na uchaguzi kutoka kwa vyama visivyoridhishwa na mwenendo wa uchaguzi wa 2005. Hadi mwisho wa 2007, kesi 27 ziliamuliwa – 26 kwa maslahi ya mshtaki moja kwa maslahi ya mshtakiwa. Kesi tano zilifutwa kwa kushindwa kukidhi masharti ya kisheria; na nne zinasubiri mahakamani.

Takriban asilimia 44 ya watu walioko gerezani ilijumuisha walioko kizuizini na wafungwa walioko rumande. Watu walioko kizuizini walioshtakiwa kwa makosa ya uhaini kwa ujumla walisubiri miaka kadhaa kabla ya kusikilizwa kwa kesi zao kutokana na muda wanaochukua polisi kukamilisha upelelezi, ukosefu wa majaji wa kusikiliza kesi, na bajeti finyu katika mahakama. Uombaji hongo wa polisi na viongozi wa mahakama ulicheleweshа kusikilizwa kwa kesi kwa wale ambao hawakumudu kulipa.

Ukaaji kizuizini wakati mwingine ulizidi hukumu iliyotolewa kwa uhalifu. Wachunguzi walikadiria kuwa takriban asilimia 5 ya watu waliowekwa rumande hatimae walitiwa hatiani, na mara nyingi wale waliotiwa hatiani tayari walikuwa wameshatumikia hukumu zao kamili kabla ya kesi zao kusikilizwa. Kiongozi mmoja wa serikali alikadiria kuwa ilichukua miaka mitano kwa kesi za mauaji kufika mahakama kuu. Kwa mujibu wa makala ya Machi 19 katika The Guardian, baadhi ya watuhumiwa walikaa miaka mingi hadi 15 gerezani bila ya kesi zao kusikilizwa mahakamani.

Mnamo Julai 2006 Waziri wa Sheria na Masuala ya Katiba alitoa agizo la kuzitaka mahakama za Sheria kumaliza kesi zote zilizopo za jinai na za madai ndani ya siku 60 ili kupunguza idadi ya kesi zinazosubiri mahakamani. Kwa sababu ya kurundikana kwa kesi na upungufu wa wafanyakazi na mahakimu, mahakama hazikuweza kufikia lengo.

**e. Kunyimwa Haki ya Kusikiliziwa**

Katiba inaruhusu mahakama huru; hata hivyo, mahakama iliendelea kukabiliwa na upungufu wa wafanyakazi, rushwa, kukosa ufanisi, na ushawishi wa wakubwa. Rushwa ilienea hususan miongoni mwa viongozi na makarani wa mahakama.

Wachunguzi huru walihoji uwezo wa mfumo wa kusikiliza kwa haraka na kwa haki kesi ya mshtakiwa. Makarani wa mahakma walichukua hongo katika kuamua ama kufungua au kutokufungua kesi na kuficha au kuelekeza vibaya majalada ya watuhumiwa wa uhaini. Kulingana na ripoti za magazeti, mahakimu wa mahakama za chini mara chache walipokea hongo katika kuamua kama mtu ana hatia au hana; kupitisha hukumu, au kuamua rufaa za kesi zinazotoka kwenye mahakama za mwanzo kwenda mahakana za wilaya. Mnamo Desemba 7, toleo la Nipashe liliripoti kuwa Taasisi ya Kuzuia Rushwa ilimkamata Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Temeke, aliyeshtakiwa kwa kuomba hongo ya takriban $ 3,600 (shilingi milioni 4) kutoka kwa mtu aliyekuwa na kesi. Gazeti hilohilo liliripoti kukamatwa kwa hakimu mwingine wa Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Kisutu aliyeomba hongo ya $ 50 (shilingi 60,000) kutoka kwa mshtakiwa.

Idara ya Sheria ilikabiliwa na upungufu mkubwa wa majengo ya mahakama. Mnamo Aprili, Ofisa Mwandamizi Mkuu wa Mahakama jijini Dar es salaam alinukuliwa na gazeti akiwaambia viongozi wa sekta ya urekebishaji sheria kuwa mikoa minane ya humu nchini haikuwa na mahakama kuu. Kwa kiasi kidogo tatizo hili lilishughulikiwa kwa kuwa na majaji na wanasheria waendesha mashtaka na watetezi ambao walizunguka katika mikoa husika, lakini gharama ya usafiri ya kwenda mahakama ya karibu zaidi ilikuwa kubwa mno.

Mfumo wa Sheria ulizingatia Sheria zisizoandikwa za Uingereza na unatambua sheria za jadi na Sheria za kiislamu katika kesi za madai. Katika masuala ya jinai Wakristo na Waislamu wote hutawaliwa na Sheria zilizotungwa Bungeni na Sheria zisizoandikwa.

Tume ya Huduma ya Mahakama, chini ya uenyekiti wa Jaji Mkuu wa Mahakama ya Rufaa, iliteua majaji wote isipokuwa wale wa Mahakama ya Rufaa na wa Mahakama

Kuu ambao waliteuliwa na Rais. Mahakama zote, pamoja na Mahakama za Kiislamu za Zanzibar, zilikuwa na wafanyakazi wa kawaida.

Nchi ina mfumo wa ngazi tano wa mahakama ambao Mahakama ya Rufaa ndiyo ngazi ya juu kabisa. Zaidi ya haya, Zanzibar ambako asilimia 95 ya watu wake ni waislamu, upo mfumo wa Mahakama za Kadhi wenye mpangilio wake ambao kilele chake ni Mahakama ya Rufaa ya Kadhi. Mahakama hizi husikiliza masuala yanayohusu sheria ya jadi ya Kiislamu katika masuala ya familia na mambo yanayohusiana na hayo. Tanzania bara, sheria ya haki za raia karibu hutawala watu wote wanaohusika katika kesi za utunzaji watoto na talaka. Sheria ya Kiislamu na ya jadi inatawala mambo mengine ya kifamilia. Kwa Waislamu na Wakristo kwa mfuatano huo. Huko bara watu wote, wakiwa wanajumuisha waislamu wako chini ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, ambayo ni mkusanyiko wa sheria ya familia inayotambua ndoa za Kiislamu na za Jadi lakini huziweka chini ya kanuni ya serikali na ulinzi wa sheria ya madai kwa ajili ya wanawake.

Ingawaje majaji wengi wa Zanzibar walikuwa Waislamu, walikuwepo pia majaji Wakristo; baadhi ya vikundi vya Kiislamu vilinung'unika ya kwamba haikuwa sahihi kwa majaji Wakristo kusimamia Sheria ya Kiislamu katika masuala ya kifamilia bila ya kupata mafunzo ya sheria ya kiislamu. Viongozi wa BAKWATA, ambalo ndilo Baraza linalosimamia masuala ya Kiislamu bara, waliomba kuanzishwe Mahakama ya Kadhi kwa ajili ya bara, hali ambayo iliibua mjadala mkali baina ya Viongozi wa Kiislamu na Maaskofu wa Kikatoliki. Maaskofu walimtahadharisha rais dhidi ya kuruhusu uanzishwaji wa mahakama hiyo. Hadi mwisho wa mwaka mabishano yaliendelea kuhusu suala hilo.

Kulikuwa na mahakama moja ya watoto, ilikuwa imeelemewa na mzigo mkubwa na ilishughulikia kesi za watototowa jijini Dar es salaam tu. Watoto wahalifu katika mikoa mingine mara nyingi kesi zao zilisikilizwa kwenye mahakama za watu wazima.

Aidha sheria inaruhusu Mahakama ya Biashara, Mahakama ya Ardhi, Mabaraza ya Nyumba na Mahakama za Kijeshi. Mahakama za kijeshi hazisikilizi kesi za raia, lakini washitakiwa wa Mahakama ya Kijeshi wanaweza kukata rufaa kwenye Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa.

**Taratibu za Usikilizaji wa Mashtaka**

Kwa kawaida usikilizaji wa mashtaka ya jinai ulikuwa wazi kwa umma na vyombo vya habari, isipokuwa kwa baadhi ya mashtaka. Mahakama ziliendesha mashtaka kwa siri kama vile kesi za usafirishaji wa dawa za kulevya.... kwa kawaida zilitakiwa kutoa sababu za kufanya hivyo. Katika kesi zinazowahusu watuhumiwa wa ugaidi; sheria inataja kuwa kila mtu isipokuwa pande husika wanaweza kuondolewa na maelezo kuweza kufichwa kwa kuwalinda mashahidi.

Majopo ya wanasheria hayatumiki. Sheria inataja dhana ya kutokuwa na kosa. Washtakiwa au wanasheria wao huweza kupata ushahidi unaoshikiliwa na serikali, haki ya kuwahoji mashahidi, na haki ya kuwasilisha ushahidi kwa niaba ya mshtakiwa.

Washtakiwa wote wanaoshtakiwa kwa masuala ya madai au jinai – isipokuwa pande zinazofikishwa mbele ya Mahakama za Kadhi na kesi zinazochunguza hali ya sheria ya kikatiba ya Zanzibar ... wanaweza kukata rufaa kwenye Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa. Sheria inataja haki ya ushauri huru kwa washtakiwa waliotuhumiwa kwa mauaji na uhaini pamoja na washtakiwa fukara kwenye kesi nyingine nzito. Washtakiwa wengi fukara walioshtakiwa kwa makosa madogo hawakuwa na ushauri wa kisheria.

Kulikuwa na mamia kadhaa ya wanasheria waendesha mashtaka nchini, ingawaje idadi iliendelea kuongezeka. Washtakiwa katika maeneo ya mijini ambao hawakuweza kukodi wakili au mwanasheria walijiwakilisha wenyewe mahakamani, lakini wanawake na watu wenye shida waliruhusiwa kupata msaada wa kisheria. Serikali iliamua kutoa uwakilishi wa kisheria kwa vikundi visivyo na uwakilishi wa kisheria kwa kuwataka wanasheria kushughulikia idadi maalum ya kesi zilizopewa msaada wa kisheria kwa kuzingatia mgawanyiko mpana wa kijiografia. Sheria inakataza mawakili kujitokeza au kuwatetea wateja katika mahakama za kiwango cha mwanzo.

**Wafungwa wa Kisiasa na Waliotiwa kizuizini**

Hapakuwa na ripoti ya kuwepo kwa wafungwa wa kisiasa au waliotiwa kizuizini.

**Taratibu na Urekebishaji katika Mahakama ya Jinai**

Upo mfumo huru na usio na upendeleo wa mahakama katika masuala ya madai. Taratibu za madai zinaendeshwa katika mahakama kuu au katika ngazi ya mahakama ya Hakimu Mkazi au Wilaya. Watu wanaweza kuleta kesi mahakamani zinazodai uharibifu au kusimamisha ukiukaji wa haki za binadamu; hata hivyo, taratibu za mahakama za madai zilikwenda polepole, hazikuwa na ufanisi, na rushwa.

**f. Uingiliaji Kiholela wa Faragha, Familia, Kaya au Mawasiliano**

Kwa ujumla Sheria inakataza kufanyika kwa vitendo kama hivyo bila ya kibali cha upekuzi; hata hivyo serikali haikuheshimu kukatazwa huko. Ni mahakama tu ndizo zinazoweza kutoa vibali kama hivyo; hata hivyo, sheria inaidhinisha pia upekuzi wa watu na maeneo bila ya kibali kama ni lazima ili kuzuia upoteaji au uharibifu wa ushahidi unaoambatana na kosa, au kama hali ni mbaya na ya haraka. Hata hiyo, katika mwaka, vikosi vya usalama viliongeza utafutaji wa vibali na mara nyingi walipekua nyumba binafsi na biashara mbele ya viongozi wa Serikali ya Mtaa na viongozi wengine. Sheria inayohusiana na ugaidi inaruhusu maofisa polisi wa ngazi za juu kufanya upekuzi bila kibali katika matukio ya dharura. Hakukuwepo na ripoti zinazoonyesha kuwa sheria hiyo imeshawahi kutekelezwa kwa vitendo.

Iliripotiwa kuwa vikosi vya usalama vilifuatilia simu na mawasiliano ya raia na wasio raia.

Katika mwaka huo serikali iliamua kuwa isingewalipa fidia na kuwapatia makazi mapya wanakijiji 135 waliodai kuwa waliondolewa kinyume cha sheria kutoka katika ardhi na nyumba zao na maofisa wa wilaya mwaka 2001. Kesi hii iliandikishwa mwaka 2005

baada ya serikali kushindwa kushughulikia uamuzi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ambao uliipa serikali siku 30 kuwalipa fidia na kuwapa makazi mapya wanakijiji hao. Kwa kuwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora haikuwa na uwezo wa kutekeleza sheria, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu cha AISE kilifungua mashtaka dhidi ya serikali; ambayo hadi mwisho wa mwaka yalikuwa yakisubiri uamuzi.

**Sehemu ya 2: Kuheshimu Uhuru wa Mtu kufanya atakacho, ikiwa ni pamoja na:**

**a. Uhuru wa kusema na wa Vyombo vya Habari**

Katiba inaruhusu uhuru wa kusema lakini haitaji kwa uwazi uhuru wa vyombo vya habari; kwa kawaida serikali ya muungano kwa sehemu inaweka mpaka kwa uhuru wa vyombo vya habari, lakini masharti ya serikali kuhusu uhuru wa vyombo vya habari yamelegezwa chini ya uongozi wa Rais Kikwete. Serikali ya bara, iliruhusu wapinzani wa kisiasa kuwasiliana na vyombo vya habari bila masharti. Katika kutiwa moyo na msaada wa Rais kwa uhuru wa vyombo vya habari; Vyombo vya habari vinaweza kuwafichua viongozi wala rushwa kwa uwazi zaidi. Kwa mfano, mwezi Machi gazeti binafsi liliandika kuhusu mwanadiplomasia wa ngazi ya juu aliyeteuliwa kwenda Italia ambaye alituhumiwa na mamlaka kwa ubadhirifu wa Dola za Kimarekani milioni 3 (shilingi bilioni 3.8).

Ingawaje hapo mwanzo vyombo vya habari vilikuwa vikidhibitiwa Zanzibar, wapinzaji wa serikali walitumia vyombo vya habari pia. Hata hivyo, vyombo vya uchapaji vilikabiliwa na baadhi ya masharti ya serikali; kwa mfano, kibali kilihtajika katika kuripoti shughuli za polisi au magereza. Serikali ilipewa mamlaka ya kuyatoza faini na kuyasimamisha magazeti chini ya Sheria ya Magazeti. Kwa kutishwa na Sheria za kashifa zinazosababisha kutolewa kwa adhabu za jinai, waandishi wa habari walijidhibiti wenyewe.

Katika mwaka huo muungano wa wadau wa vyombo vya habari walikosoa pendekezo la serikali la kuwasilisha miswada yake ya habari na huduma za vyombo vya habari; kwa kuogopa kuwa miswada hiyo ilikusudiwa kuipa serikali udhibiti mkubwa.

Huko bara, mhariri mkuu wa gazeti la Citizen alilazimika kwenye toleo la Januari 23 kuwa Sheria ya Siri za Viongozi iliwafanya kuwa wahalifu wote wawili, mwandishi wa habari na mtoa habari, hata kama taarifa iliyoenezwa haina athari yoyote.

Zanzibar, ambayo ilikuwa na sera ya vyombo vya habari tofauti na ya bara, sheria zinazoweka mipaka kwa uwezo wa vyombo vya habari kufanya kazi kwa ufanisi na kukosa ufanisi kwa mahakama kulipunguza uhuru wa kusema na wa vyombo vy habari. Mnamo Aprili, sheria mpya ya kinga, ulinzi na haki za wajumbe wa Baraza la wawakilishi ilipitishwa, ikibatilisha kibali cha jumla ambacho vyombo vya habari vilikuwa nacho cha kuhudhuria vikao vya Baraza na kuidhinisha hukumu ya kifungo cha hadi miaka mitatu gerezani na faini ya dola za kimarekani zisizopungua 250(shilingi 300,000) kwa kuchapisha kashfa zilizohusu wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tabia au

taarifa zao. Hakukuwepo na kesi za kukamatwa au adhabu zilizoripotiwa chini ya sheria hii katika mwaka huo.

Sheria inavitaka vyama vya siasa kuunga mkono Muungano wa Tanzania (baina ya Tanganyika na Zanzibar), na watu wanaotumia lugha ya "matusi" kuhusu uongozi wa nchi kukamatwa. Masharti haya hayakutumiwa katika mwaka huo, hata hivyo, kulikuwa na mifano mingi ya viongozi wa taifa waliokosolewa vikali kwenye magazeti, hususan kuhusiana na rushwa.

Usajili wa magazeti uliendelea kuwa mgumu na ulitegemea utashi wa msajili

Stesheni za redio na televisheni zote isipokuwa moja zilimilikiwa na watu binafsi. Kulikuwa na masharti ya serikali yanayofanana. Kwa mfano, stesheni za redio hazikuweza kutangaza kwa lugha za kikabila.

Kulingana na idara ya maelezo ya Zanzibar, wakala wa serikali, mojawapo ya magazeti mawili ya Zanzibar ilimilikiwa binafsi, na moja lilimilikiwa na serikali. Serikali ilidhibiti maudhui ya matangazo kwenye redio na televisheni, ikiwa ni pamoja na vituo vilivyomilikiwa na watu binafsi.

Kesi ya tuhuma ya mwaka 2005 ya kupigwa na viongozi wa magereza na nyingine za mpiga picha Mpoki Bukuku na mwanaharakati wa haki za binadamu na mtoa habari Christopher Kidanka zililetwa kusikilizwa katika mwaka na hadi mwisho wa mwaka zilikuwa zikisubiri uamuzi. Waandishi wa habari walijaribu kuandika habari ya familia zilizoondolewa kwenye nyumba zilizokuwa zikimilikiwa tena na idara ya magereza. Hivi karibuni waandishi wote wawili waliishitaki idara ya magereza kwa fidia.

Mnamo Aprili 2006 watu wasiofahamika walitishia kuwaua wahariri na waandishi wa habari wa gazeti la This Day, wakiwaonya dhidi ya utoaji taarifa kuhusu rushwa katika taasisi za umma. Mhariri wa gazeti hilo aliuambia mkutano wa vyombo vya habari kuwa mtu mmoja aliwapa waandishi wa habari dola za kimarekani takriban 20,000 (shilingi milioni 25.5) ili kuacha kuchapisha habari zilizochunguzwa kuhusu maovu katika jamii. Kwa mujibu wa This Day la Julai 25, mwandishi wa habari, Mbaraka Islam, anayefanya kazi za wachapishaji wa This Day, aliripoti kuwa alipokea mfululizo wa vitisho vya kuuawa, na kwamba hii haikuwa mara ya kwanza kwa watoa habari wa This Day kupokea vitisho vya aina hiyo. Magazeti ya Guardian ya Machi 19 na Mwana Halisi la Machi 21-27 yaliripoti pia kwamba ndugu wa ofisa mwandamizi serikalini aliyeshtakiwa kwa mauaji waliwashambulia waandishi wa habari waliokuwa wakijaribu kumpiga picha mtuhumiwa. Kwenye makala ya Mwana Halisi, mwananchi mmoja alikosoa polisi kwa kutokuchukua hatua dhidi ya ndugu hao kabla au baada ya vipigo. Mnamo Machi 10 Guardian, wataalamu wa Sheria na wanaharakati wa haki na binadamu walishutumu pia polisi na wakala wa usalama kwa kusimama pembeni wakati waandishi wa habari walipokuwa wakipigwa katika maeneo ya mahakama.

Mamlaka ilifuta mashtaka dhidi ya wafuasi wawili miongoni mwa watatu wa Chama cha Wananchi (CUF) waliotuhumiwa kuwashambulia waandishi wa habari mjini Dar es

Salaam mwaka 2005. Kesi ya mshtakiwa wa tatu ilipelekwa kusikilizwa lakini hadi mwisho wa mwaka ilikuwa ikisubiri uamuzi.

Mamlaka za Zanzibar ziliendelea kuweka vizuizi. Kwenye shughuli za maripota mwezi Agosti serikali ilikataa kutoa ruhusa kwa kikundi cha nje cha watangazaji wa redio cha Idhaa ya BBC kurusha programu hizo kutoka Zanzibar wakati wa kipindi cha Kutana-na-Wasikilizaji wa Kanda. Idhaa ya BBC ilikuwa imerusha vipindi kama hivyo kutoka bara na nchi jirani. Tarehe 10 Septemba, viongozi waliwakamata waandishi watatu wa habari huko Pemba walipokuwa wakitoka katika kijiji walimokuwa wakifanya uchunguzi kuhusu upungufu wa chakula.

Kitisho cha utumiaji wa sheria inayohusu kashifa, ambayo hutoa adhabu za makosa ya jinai, kiliwatia hofu baadhi ya waandishi wa habari na kuwafanya wengi kuzingatia tathmini binafsi. Hata hivyo, mnamo Septemba 27, Mwanahalisi lilitangaza kuwa watu ambao hawakufahamika walikuwa wakitishia kampuni ya Printech ya uchapaji wa gazeti hilo na gazeti lililokuwa na kashfa na kulifunga kwa sababu ya makala za uchunguzi lilizochapisha. Wakati sheria inataja kuwa mshitakiwa lazima athibitishe kusudio la uovu, wachunguzi wengi wa vyombo vya habari waliikosoa mahakama kwa kudharau kifungu hiki na kutoa adhabu kali kwa vyombo vya habari, na uzito zilizokuwa zimechochewa kisiasa. Hata hivyo, hapakuwa na taarifa ya matukio maalum ya vitendo hivyo katika kipindi cha mwaka huu, kwa mujibu wa Baraza la Vyombo vya Habari, asasi za mafunzo, na waandsihi wa habari.

Huko Zanzibar vyombo vya habari kutokupata taarifa za serikali limeendelea kuwa ni tatizo kubwa. Serikali ilitaja usalama wa raia kama kisingizio cha kuficha maoni ambayo iliyaona hayakubaliki kisiasa. Kanuni za utumishi wa umma zinaruhusu tu wawakilishi wa ngazi ya juu wa serikali kutoa taarifa kwenye vyombo vya habari.

Toleo la Februari 1 la Citizen liliripoti kuwa Serikali ilipiga marufuku matangazo na machapisho ya Haki Elimu, AISE ya kitaifa ambayo ilikuwa ikikosoa utendaji wa serikali katika sekta ya elimu. Hata hivyo, toleo la Februari 8 la The Guardian liliripoti kuwa serikali iliondoa adhabu hiyo baada ya mkutano baina ya Waziri Mkuu na Mkurugenzi wa Haki Elimu.

Kulingana na taarifa iliyotolewa na tawi la Tanzania la Taasisi ya Vyombo vya Habari ya Kusini mwa Afrika, uhuru wa vyombo vya habari nchini Tanzania uliendelea kudhoofika kutokana na ukosefu wa mafunzo ya kutosha, mishahara midogo, na rushwa katika taaluma ya uandishi wa habari. Kwa mfano, toleo la Septemba 28 la This Day liliripoti kuwa mkutano wa wahariri uliofanyika Dar es Salaam uliwashutumu wahariri na waandishi wa habari wenzao kwa kulipwa pesa na wafanyabiashara na wanasiasa maarufu. Aidha waliwashutumu wenzao kwa kuhongwa kazi za kisaisa, na kuongeza kuwa wale walioripoti rushwa ya hali ya juu walikabiliwa na vitisho wao binafsi na ajira zao.

**Uhuru wa Intaneti:**

Hapakuwa na vizuizi vya serikali kuhusu upatikanaji wa intaneti au ripoti za serikali kufuatia baruapepe au maeneo ya mazungumzo. Watu binafsi na vikundi waliweza kushiriki katika utoaji wa maoni yao kwa amani kupitia kwenye intaneti ikiwa ni pamoja na kupitia baruapepe. Idadi ya vibanda vya intaneti na watoaji wa huduma ya intaneti iliongezeka katika kipindi cha mwaka huu. Hata hivyo ni asilimia 10 tu ya wananchi ndiyo iliyokuwa ikipata umeme na hivyo kuwa kipingamizi kikubwa sana cha upatikanaji wa huduma hizi kwa ujumla.

**Uhuru wa Kitaaluma na Matukio ya Utamaduni**

Hapakuwa na vizuizi serikalini kuhusu uhuru wa kitaaluma au matukio ya utamaduni.

**b. Uhuru wa Kukusanyika kwa Amani na Haki ya Kujiunga na Chama**

**Uhuru wa kukusanyika**

Katiba inaruhusu uhuru wa kukusanyika, na kwa ujumla serikali ililiheshimu haki hizi kwa vitendo.

Serikali inawataka watayarishaji wa mikutano kupata kibali cha polisi kabla. Polisi wana uwezo wa kukataa kutoa kibali kwa sababu ya usalama wa raia au kwa misingi ya usalama au iwapo anayetafuta kibali hicho ni mwanachama wa shirika au chama cha kisiasa ambacho hakijasajiliwa.

**Uhuru wa kujiunga na Chama**

Katiba inaruhusu kuwepo kwa uhuru wa kujiunga na chama na kwa ujumla serikali iliheshimu haki hii kwa vitendo, ingawa serikali iliendelea kuweka masharti katika kusajili vyama vya siasa. Vyama vilivyosajiliwa vilizuiwa kusimamisha wagombea katika uchaguzi wa hivi karibuni 2005.

Ripoti za vyombo vya habari za mwezi Oktoba zilisema kuwa mbunge wa upinzani bungeni, Zitto Kabwe, hakuruhusiwa kuhutubia wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam alikoitwa kuwasilisha makala. Kulingana na Guardian la Oktoba 5 Chama cha Wanafunzi wa Sayansi ya Siasa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Programu ya Mtandao wa Wanafunzi Tanzania waliulaumu uongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kuharibu mipango yao ya kumwalika Kabwe, kwa kutaka hatua zichukuliwe kwa tatizo hilo lililochochewa kisiasa. Chuo Kikuu ni taasisi ya umma.

**c. Uhuru wa Dini**

Katiba inaruhusu uhuru wa dini hata hivyo kulikuwa na mipaka katika uhuru wa dini

Serikali inavitaka vikundi vya dini viandikishwe Wizara ya Mambo ya Ndani. Ili kusajili kikundi cha dini lazima wawepo angalau wafuasi 10 na lazima kuwasilisha

katiba, tawasifu ya viongozi wake na barua ya mapendekezo kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya mahali patakapokuwa maskani ya kikundi hicho. Vikundi vya Kiislamu vya bara vilitakiwa pia kuwasilisha barua kutoka BAKWATA, baraza linalosimamia masuala ya Uislamu ya bara, na kwa upande wa Zanzibar, barua ya Mufti. Asasi hizi zinapendekeza kuidhinishwa au kutokuidhinishwa kwa usajili na Msajili Mkuu wa Serikali Katika kipindi cha mwaka huu hapakuwa na ripoti kwamba serikali ilikataa kusajili kikundi chochote bara; mwaka 2006 huko Zanizbar Mufti alipendekeza kutokusajiliwa kwa vikundi viwili, kikundi cha Ahmadiya na kikundi cha Bahai, kwa sababu ya upinzani unaodaiwa kuwepo baina ya imani zao na imani za Kiislamu. Kikundi cha Ahmadiya kilifungua mashtaka dhidi ya Ofisi ya Mufti kutokana na pendekezo hilo. Katika mwaka huo mahakama ilifuta kesi kutokana na kukosekana kwa ushahidi.

Sheria inakataza kuhubiri au kutawanya vitu vinavyodhaniwa kuchochea au kutishia usalama wa raia. Mwaka 2006, mara kwa mara serikali ilikataa maombi ya vikundi vya dini vya kutaka kufanya maandamano kwa sababu ya uwezekano kwamba mkusanyiko ungeweza kusababisha mapambano au kuchochea mgogoro wa kidini. Kulingana na toleo la Juni 26 la Al Huda, Polisi wenye silaha walivunja mkutano wa dini ya Kiislamu eneo la Madizini katika wilaya ya Turiani, mkoa wa Morogoro, ambapo kulikuwa na mabishano kuhusu dini kati ya Mtumishi wa Kiislamu na Mchungaji wa Kikristo. Baada ya mkutano wa saa mbili na maofisa wa polisi, waislamu waliruhusiwa kuendelea na mkutano wao siku iliyofuata.

Hakukupatikana taarifa kuhusu kesi ya mhubiri wa Kikristo Cecil Simbulanga, aliyekamatwa mwezi Agosti 2006 kwa "Kuhubiri uchochezi" ambao uliwakashifu Uislamu. Baada ya kuachiwa kwa dhamana, Simbulanga alikamatwa tena mwezi Desemba 2006 kwa kuukashifu Uislamu wakati akihubiri, na safari hiyo alishikiliwa bila dhamana.

Katika mwaka huo wawakilishi wa Waislamu waliiomba serikali kuanzisha Mahakama za Kadhi na sheria ya Sharia bara kwa ajili ya kuamua masuala ya Kiislamu. Vikundi vya Kikristo vimepinga kuwa mahakama hizo zitakiuka hali ya serikali ya kutokuwa upande wowote miongoni mwa dini mbalimbali na kwamba Katiba ya Muungano haikueleza Mahakama ya Kadhi kitaifa. Mwishoni mwa mwaka jambo hilo lilikuwa likifuatiliwa lakini lilibakia bila kuamuliwa.

**Unyanyasaji wa Kijamii na Ubaguzi**

Ingawa uhusiano miongoni mwa dini mbalimbali katika jamii kwa ujumla umekuwa wa kirafiki, kumeendelea kuwa na mvutano kati ya Waislamu na Wakristo na taarifa za fujo za kijamii za kidini. Kwa Tanzania bara, gazetri la Msema Kweli la Mei 27 liliripoti kwamba watu wasiotambulika walichoma moto mali za Kanisa la Evangelical Assemblies of God la Wilaya ya Kigambombi, mkoa wa Dar es Salaam.

Gazeti la Nyakati la Julai 22 liliripoti kwamba tarehe 5 Julai watu wasiofahamika walichoma moto Kanisa la Free Pentecostal huko Kusini Unguja, Zanzibar. Mchungaji

William Bombey, aliwaeleza waandishi wa habari kuwa kanisa lake limekuwa likitishiwa mara kadhaa na kwamba viongozi wa Serikali ya Mitaa waliliomba kanisa kuhama na kwamba mtu yeyote aliyetaka kuuza ardhi kwa kanisa aliitwa na Serikali ya Mtaa na kutishiwa. Mchungaji alieleza kwamba waumini wa kanisa walichoshwa na kutoruhusiwa kutumia kanisa na kuzuiwa kuabudia ndani ya jengo tarehe 1 Julai; siku nne baadaye, kanisa liliteketezwa.

Sera ya Serikali inakataza ubaguzi dhidi ya mtu yeyote kwa misingi ya imani au taratibu za dini; hata hivyo, vikundi vya waislamu vinaendelea kudai kuwa serikali inawabagua katika shughuli za ajira, elimu na utekelezaji wa sheria. Vikundi vya Wakristo vililalamika kwamba serikali ilitoa nafasi zote nyeti serikalini kwa Waislamu.

Kulikuwa na ripoti kwamba, katika mikutano kadhaa ya Waislamu katikati ya miji, baadhi ya washiriki wanaukosoa Ukristo hadharani, ambapo mara moja moja husababisha kugombana. Majira la Septemba 16 liliripoti kwamba Waislamu na Wakristo huko Arusha walitupiana mawe na vifaa vyenye ncha katika Mkutano wa Wakristo ambapo Wakristo walikuwa wanasikiliza hadharani kanda ya kaseti iliyokuwa inadhihaki Kurani. Polisi walizima vurugu; mtu mmoja ambaye hakutambulika aliumizwa.

Kwa Tanzania bara vyombo vya habari viliripoti kuwa Mwalimu wa Shule ya Sekondari Tanga alituhumiwa kutoa kauli za dharau dhidi ya Mtume Mohammed na kuwaeleza wanafunzi wake kwamba dini ya Kiislamu inawanyanyasa wanawake wa Kiiislamu. Gazeti la Nyakati toleo la Agosti 12 liliripoti kwamba Wizara ya Elimu ilimsimamisha kazi Mwalimu huyo na kuwa mashehe kadhaa waliomba kwamba akatwe kichwa kwa kuukashifu Uislamu.

Idadi ya Wayahudi ilikuwa ndogo sana; hapakuwa na ripotiza vitendo vya uhasama dhidi ya wayahudi.

Kwa majadiliano ya kina, tazama Ripoti ya Kimataifa ya Uhuru wa Dini ya 2007.

**d. Uhuru wa Kutembea wa Wakimbizi wa Ndani ya nchi, Ulinzi wa Wakimbizi na Watu wasio na Uraia wowote.**

Katiba inaeleza uhuru wa kutembea ndani ya nchi, safari za nje, uhamaji na urejeshaji nyumbani, na kwa ujumla serikali inaheshimu haki hizi kwa vitendo; hata hivyo, uzembe usiofaa na ruhswa vinazuia utekelezaji, na kulikuwa na upotoshaji wa mara kadhaa katika kuheshimu haki ya mahali pa hifadhi. Serikali ilijitolea kushirikiana na ofisi ya UNHCR na Mashirika ya hisani katika kutoa ulinzi na msaada kwa wakimbizi wa ndani ya nchi; wakimbizi, wakimbizi wanaorejea makwao, wanaotafuta hifadhi, watu wasio na uraia wowote na watu wengine wenye matatizo. Serikali inawakamata na kuwafukuza nchini baadhi ya wahamiaji haramu.

Polisi katika vituo vya ukaguzi wakati mwingine wanaomba rushwa.

Sheria hairuhusu uhamishaji kwa nguvu wa raia, na serikali haifanyi uhamishaji wa nguvu.

**Ulinzi wa Wakimbizi**

Sheria inatoa haki ya kuwapa hadhi wakimbizi au hifadhi kwa mujibu wa Mkataba wa UN wa 1951 kuhusiana na Hadhi ya Wakimbizi na protokali yake ya 1967, na serikali imeanzisha mfumo wa kutoa ulinzi kwa wakimbizi. Kwa kawaida serikali inatoa ulinzi dhidi ya "uonevu," kurudi kwa watu katika nchi ambako kulikuwa na sababu ya kuamini walihofia kuadhibiwa. Katika mwaka huo serikali ilitoa hadhi ya ukimbizi na kuanza mchakato wa kubainsiha ni wakimbizi wapi wana sifa za uraia. Vigezo vilijumuisha muda wa kukaa nchini na kama mkimbizi ana rekodi ya uhalifu au hana. Mwezi Deemba, Wizara ya Mambo ya Ndani iliunda kikosi cha makazi ya zamani ili kushughulikia hali mbalimbali za ushirikiano na wenyeji na urejeshwaji wa wakimbizi wa Burundi wa 1972.

Tofauti na mwaka uliopita, viongozi wa UNHCR waliruhusiwa kuwepo katika mpaka wa kuwachuja wakimbizi. Mara kwa mara serikali inakataa kuingia kwa wale wanaotafuta hifadhi au hadhi ya ukimbizi mpakani.

Mwaka 2006 kulikuwa na wakimbizi takriban 685,000 nchini, hasa kutoka Burundi na Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), pamoja na takriban 289,000 katika kambi 14 zinazosaidiwa na UNHCR huko Kaskazini-Magharibi. Mwaka 2006 kiasi cha 400,000 walikuwa katika makazi ya wakimbizi au vijiji vinavyojitegemea; katika mwaka huo, walibakia takriban 200,000. Hadi mwishoni mwa kipindi cha kutoa ripoti, nchi ilikuwa inawahifadhi wakimbizi takriban 400,000, hasa kutoka katika nchi za jirani. Karibu nusu yao waliishi kwa kujitegemea; wengine walipewa makazi katika kambi za msaada za UNHCR. Inabakia kutokuwa halali kwa wakimbizi kuishi nje ya kambi au makazi, au kusafiri nje ya kambi zao bila ya vibali, isipokuwa kutafuta kuni ndani ya maili mbili na nusu kutoka kambini kwao. Kwa kawaida wanawake na watoto wanaposafiri mbali na kambi zao kwenda kutafuta kuni, mara nyingi wanakabiliwa na wizi, unyanyasaji wa kimwili na kubakwa. Idadi ya matukio imepungua baada ya viongozi kuomba wakimbizi wasafiri katika makundi.

Mwaka 2006 wakimbizi waliokamatwa nje ya maeneo waliyotengewa bila ya vibali, hasa maeneo ya mjini kama vile Dar es Salaam, walikamatwa na kufungwa hadi miezi sita au kulipa faini ya kiasi cha $ 39 (shilingi 50,000). Mwaka huo kiasi cha wakimbizi 1,000 na wanaotafuta hifadhi nje ya kambi bila ya vibali walishtakiwa kwa kutofuata sheria chini ya sheria ya uhamiaji walihukumiwa kifungo cha miaka miwili kikifuatiwa na kufukuzwa katika nchi wanakoomba hifadhi. Hata hivyo, katika mwaka huo, serikali ililegeza mkabala wake kwa ukiukaji mdogo wa sheria unaofanywa na wakimbizi, kuwashtaki chini ya sheria inayoshughulikia wakimbizi, ambayo inataka kushikiliwa kwa siku tatu au kuhudumia jamii, au vyote viwili. Kadri ya wakimbizi 100 walikamatwa nje ya maeneo yaliyotengwa katika mwaka huo na wote walihukumiwa kuhudumia jamii kuliko kifungo.

UNHCR kwa kushirikiana na serikali imeendelea kutoa ulinzi wa wakimbizi; hata hivyo, uhalifu ikiwemo mauaji, unyang'anyi, ubakaji na unyanyasaji majumbani – limeendelea kuwa tatizo kubwa ndani na jirani na kambi za wakimbizi. Kwa mfano, gazeti la Daima toleo la Oktoba 15 liliripoti kwamba wakimbizi wa Burundi 19 pamoja na wahamiaji haramu wanne walikamatwa huko Mpanda, Rukwa kwa kuwa nje ya makambi yao bila ya vibali halali. Ibara inasema wakimbizi wawili walikamatwa kwa kushiriki katika unyang'anyi wa kutumia silaha. Mwezi Aprili viongozi wa UNHCR huko Kasulu waliripoti mfululizo wa matukio ya ujambazi wa kutumia silaha katika kambi za Warundi. Aprili 11, majambazi watatu wenye silaha walivunja nyumba ya mkimbizi Mrundi huko Mtabila, wakamuua na kuiba kiasi cha $150 (shilingi 150,000) alizokuwa nazo mke wake.

Tarehe 18 Aprili, majambazi wawili walivunja nyumba ya mkimbizi Mrundi katika kambi ya Muyovisi na kuchukua kiasi cha $160. Aprili 23, majambazi wawili walimnyang'anya mkimbizi katika kambi ya Muyorozi $15 (shilingi 20,000).

Katika mwaka huo, serikali ilichunguza, kuwashitaki na kuwaadhibu wanyanyasaji katika kambi za wakimbizi, lakini kesi nyingi zinazohusisha uhalifu na unyanyasaji nje ya makambi zilipelekwa kwa viongozi wa nchini. Makazi ya wakimbizi yaliathiriwa vibaya na ucheleweshaji na kutokuwa na mahakama za kutosha, matatizo ya kawaida yanayowakabili raia. Kulikuwa na ripoti kwamba baadhi ya wakimbizi wanajihusisha katika haki za sungusungu ndani ya kambi, mara kwa mara wakipiga wakimbizi wengine.

Wakimbizi Warundi na Wakongo wameendelea kurejea nyumbani katika mwaka huo, wakihamasishwa na kuongezeka kwa usalama huko Burundi na DRC pamoja na kuhamasishwa na serikali na msaada wa UNHCR. Katika mwaka huo, tume ya pande tatu inayoundwa na UNHCR na serikali za Tanzania na Burundi ilihamasisha urejeshwaji nyumbani kwa kufunga shule 20 katika kambi na kusimamisha miradi ya wakimbizi inayozalisha kipato. Kambi tano zilifungwa katika mwaka huo. UNHCR iliwezesha urejeaji nyumbani wa hiari wa wakimbizi 38,253 Warundi, na wakimbizi 19,547 wa DRC.

UNHCR iliendelea kuwezesha urejeaji nyumbani wa wakimbizi kwa hiari kwenda DRC, na zaidi ya 26,000 walirejea nyumbani katika mwaka huo. Urejeaji wa walio wengi ulikuwa wa hiari; hata hivyo, baadhi ya wakimbizi walirejea kwa kutambua vitisho vya uonevu au vikwazo katika shughuli zao nchini Tanzania. Kwa mfano, katika mwaka huo Mkuu wa Wilaya ya Kibondo aliendelea kutembelea kambi na kuwaomba wakimbizi warejee nyumbani. Vikwazo vya wakimbizi katika kambi zao pia vilihamasisha urejeaji nyumbani.

**Sehemu ya 3: Kuheshimu Haki za Kisiasa: Haki ya Raia Kubadili Serikali yao**

Katiba inawapa raia haki ya kubadili serikali yao kwa amani, na raia wanaitumia haki hii katika chaguzi za bara na Zanzibar. Hata hivyo, masharti ya kisheria na kifedha yanayokipendelea chama tawala cha CCM, ukiukaji wa taratibu wakati wa kupiga kura na vurugu za kisiasa vinazuia ufanisi wa mchakato wa uchaguzi huko Zanzibar.

**Chaguzi na Ushiriki wa Kisiasa**

Chaguzi mbalimbali zinafanyika bara na Zanzibar, wakati mwingine kwa siku hiyohiyo ambapo raia wa sehemu mbili za Muungano wanachagua viongozi wa maeneo, wabunge wa bunge la taifa, na rais wa muungano (Taifa). Aidha, wazanzibari peke yao wanamchagua rais wa Zanzibar na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mwaka 2005, Jakaya Kikwete mgombea wa CCM, alichaguliwa kuwa rais wa Muungano kwa asilimia 80.2 za kura katika uchaguzi uliochukuliwa na waangalizi kama wa huru na haki zaidi kuliko chaguzi zilizopita; hata hivyo, kampeni zilizotangulia uchaguzi zilitawaliwa na vurugu katika baadhi ya mikoa.

Mwaka 2005, wapigakura katika visiwa huru vya Zanzibar walimchagua rais, wabunge, na wawakilishi wa maeneo kwa ajili ya visiwani. Mgombea wa CCM Amani Karume, rais aliyekuwa madarakani, alichaguliwa tena kwa asilimia 53 ya kura katika uchaguzi uliogubikwa na dosari na vurugu.

Kusumbuliwa kwa vyama vya siasa na serikali kulipungua sana katika mwaka huo ukilinganisha na uchaguzi wa mwaka 2005.

Huko Zanzibar, hasa katika kisiwa cha Pemba, wanasiasa wa Chama cha upinzani walidai kuwa serikali iliwabagua katika ajira. Serikali ilikuwa ni mwajiri mkubwa huko Zanzibar.

Watu binafsi na vyama wangeweza kuwa huru kutaja ugombea wao na kugombea uchaguzi. Sheria inataja kuwa watu wanaoendesha ofisi lazima wawakilishe chama cha siasa kilichosajiliwa, na inavitaka vyama vyote vya siasa kuunga mkono muungano na Zanzibar; pia inakataza vyama kujihusisha na ukabila, dini au uhusiano na dini.

Msajili wa vyama vya siasa ana mamlaka kamili ya kukubali au kukataa usajili wa chama chochote cha siasa na anawajibika na utekelezaji wa kanuni katika vyama vilivyosajiliwa.

Vyama vinavyopewa usajili wa muda vinaweza kufanya mikutano ya hadhara na kuandikisha wanachama ili kupata usajili kamili na kustahili kuweka wagombea kwa uchaguzi. Vyama vilivyosajiliwa kwa muda vina miezi sita ya kukabidhi orodha za wanachama angalau 200 katika mikoa 10 kati ya 26 nchini, ikiwa ni pamoja na mikoa miwili kati ya mitano ya Zanzibar.

Kutawala kisiasa kwa CCM tangu uchaguzi wa kwanza wa nchi wa vyama vingi, kwa sehemu fulani kulitokana na vikwazo vya serikali kwa upinzani wa kisiasa, lakini pia kutokuwa na mpangilio na ukosefu wa fedha wa vyama vilivyo vingi. Hata hivyo, katika mwaka huo mahakama ilianza kusikiliza rufaa mbili zilizowasilishwa na wanachama wa chama cha upinzani dhidi ya washindi wa uchaguzi wa ubunge mwaka 2005 ambao ni wagombea wa CCM, wakituhumu udanganyifu na rushwa uliofanywa na wagombea wa CCM. Gazeti la Majira la tarehe 14 Februari liliripoti kwamba rufa ya mgombea wa CUF

kwa jimbo la Musoma Mjini, imepangwa kusikilizwa Februari 19. Tarehe 24 Oktoba, Daily News liliripoti kwamba Mahakama Kuu imeanza kusikiliza rufaa ya Mgombea wa CUF Wilfred Rwakatare dhidi ya mgombea wa CCM Balozi Kagasheki kwa jimbo la Bukoba Mjini. Hadi mwisho wa mwaka kesi zote mbili zilikuwa zinasubiri uamuzi.

Sheria ya uchaguzi inataja wabunge wanaomaliza kipindi chao kupata $15,686 (shilingi milioni 20) kama "marupurupu," ambayo walio madarakani huyatumia katika kampeni ili kuwezesha kuchaguliwa kwao tena. Asasi kadhaa zisizo za kiserikali na vyama vya upinzani wanapinga sharti hilo wakisema kuwa linafanya kuwa vigumu sana kwa wanaotamani kugombea ubunge kutoka vyama vya upinzani kuingia katika ushidnani unaofaa.

Citizen la Machi 7 liliripoti rufaa ya serikali dhidi ya uamuzi wa 2006 uliotolewa na Mahakama Kuu ikiruhusu wagombea wa kujitegemea kugombea chaguzi za eneo na kitaifa. Maombi, yaliyotolewa na kiongozi wa chama cha upinzani cha Demokrasia, Mchungaji Christopher Mtikila, yalishutumu Katiba ya Sheria inayowataka wagombea kuwakilisha vyama vya siasa ili kugombea nafasi ya umma. Hadi mwishoni mwa mwaka kesi ilikuwa bado inasubiri uamuzi.

Vurugu ziliripotiwa kati ya wanachama wa CUF na kikosi cha Kuzuia Ghasia (FFU) wakati mashabiki wa chama walipokusanyika bila ya kibali cha polisi. Polisi walitumia gesi ya kutoa machozi kwa mashabiki wa upinzani na kukamata watu 23.

Sheria inataka kwamba wanawake wapate angalau asilimia 30 za viti katika bunge. Wanawake wanateuliwa na vyama vyao husika vya kisiasa ili kupata viti vilivyotengwa kwa ajili yao, kufuatana na idadi ya viti ambavyo vyama vyao vimeshinda. Baada ya chaugzi za 2005 kulikuwa na viti maalumu 75 vya wanawake, na mwishoni mwa mwaka kulikuwa na wanawake 91 katika viti 320 vya bunge. Wanawake wanashikilia viti 18 katika viti 81 vya Baraza la Wawakilishi Zanzibar na nafasi nne katika baraza la Mawaziri la Serikali ya Zanzibar. Baada ya kushika madaraka mwaka 2005, Rais Kikwete aliwateua Mawaziri wanawake saba (ukilinganisha na wanne katika utawala uliopita) na Manaibu Waziri wanawake 10. Baadhi ya wanawake hao waliteuliwa kuongoza wizara kuu ikiwa ni pamoja na mambo ya nje, fedha na sheria. Katika mwaka huo wanawake takriban saba walikuwa Majaji wa Mahakama Kuu na mwanamke mmoja alikuwa hakimu wa Mahakama ya Rufaa ya Muungano.

Kulikuwa na wabunge 11 wenye asili ya kiasia katika viti 320 vya Bunge la Taifa, mmoja akiwa kama Waziri wa Fedha.

**Rushwa na Uwazi katika Serikali**

Sheria inataja adhabu za jinai kwa rushwa ya kiongozi na kwa ujumla serikali inatekeleza sheria hii ipasavyo dhidi ya viongozi wa ngazi ya chini. Hata hivyo, wananchi waliikosoa serikali kwa kutotekeleza sheria ipasavyo dhidi ya viongozi wa ngazi ya juu wanaotuhumiwa kwa rushwa, ikionyesha kuwa viongozi hawa wanaweza kujihusisha katika vitendo vya rushwa bila kuadhibiwa.

Licha ya mafanikio katika muongo uliopita, rushwa imebakia kuwa tatizo lililoenea katika serikali nzima. Viashirio vya utawala Duniani vya Benki ya Dunia vinaonyesha kuwa rushwa ilikuwa ni tatizo kubwa. Usikilizaji wa awali wa kesi ya rushwa inayomhusisha aliyekuwa balozi wa Italia ilianza Agosti 21; hadi kufikia mwisho wa mwaka kesi ilikuwa inasubiri uamuzi. Kutokana na tatizo la tuhuma za rushwa, Novemba 16 Rais Kikwete alimteua aliyekuwa Mwanasheria Mkuu kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya kupitia upya mikataba yote ya uchimbaji madini. Wajumbe wa kamati ni pamoja na wabunge kutoka chama tawala cha CCM na kutoka upinzani, pamoja na setka binafsi na viongozi waandamizi serikalini.

Viongozi waandamizi serikalini walikadiria kuwa asilimia 20 ya bajeti ya serikali kwa kila mwaka wa fedha ilipotea kwa rushwa, ikiwa ni pamoja na wizi, udanganyifu na miamala ya uongozi ya ununuzi.

Kulikuwa na uwajibikaji mdogo katika vyombo vingi vya serikali. Hakuna sheria inayotoa nafasi kwa wananchi kupata taarifa za serikali. Viongozi wa Serikali kwa kawaida wanakataa kutoa taarifa.

Mwezi Aprili Bunge la Taifa liliridhia Muswada wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa, likiipa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mamlaka zaidi. Sheria mpya inafafanua makosa vizuri zaidi na kuongeza idadi ya makosa kutoka manne hadi 24, lakini ukosoaji kutoka AZISE na vyama vya upinzani unaeleza kuwa chini ya sheria mpya viongozi waandamizi wa serikali wanalindwa na kushtakiwa bila ya idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai; wanalalamika kwamba sharti hilo litazuia ufanisi wa sheria.

Kwa upande wa bara, Ofisa Uchunguzi Mkuu wa TAKUKURU alinukuliwa na Citizen tarehe 17 Januari akisema kwamba rushwa katika ununuzi wa umma ilikuwa bado inatolewa kiasi kikubwa licha ya kutungwa kwa sheria na kanuni za kuzuia kwa bidii. Kwa upande wa Zanzibar, Daily News la Julai 25 liliripoti kwamba wabunge kadhaa waliiomba serikali kuwashitaki viongozi wote wazanzibari waliotajwa na ripoti za mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali kuanzia 2003 hadi 2005 kwa kutumia vibaya fedha za umma na kutowajibika.

Uelewa wa wananchi wa kiwango cha rushwa miongoni mwa viongozi wa umma, wakati bado kiko juu, kinaonyesha kushuka. Toleo la Januari 29 na matoleo yaliyofuatia ya East African yaliripoti kwamba Waziri wa Fehda ameagiza uchunguzi katika ufisadi mkubwa ndani ya Benki Kuu. Tuhuma za rushwa zimeelekezwa katika gharama za ujenzi wa makao makuu ya benki na malipo ya Dola milioni 30.8 kutoka katika akaunti yake ya nje kwenda kwa kampuni inayodaiwa kuwa ya uongo. Ingawa wabunge wa upinzani walitaka kujiuzulu kwa gavana wa benki; tarehe 3 Julai, The African liliripoti kauli ya Waziri Mkuu akitangaza kwamba vyombo husika vya serikali vilikuwa vinachunguza suala hilo. Uchunguzi ulikuwa unaendelea hadi mwisho wa mwaka. Tarehe 5 Julai, gazeti la This Day liliripoti kwamba Wizara ya Ulinzi imelipa kiasi cha dola milini 20 kuzidi bei ya soko kwa ajili ya helikopta waliyoikataa awali kuwa haifai kwa matumizi.

Serikali imeendelea kutumia mashirika yenye utaalamu kupambana na rushwa katika mwaka huo, lakini ufanisi wao ulikuwa mdogo. Kitengo katika Wizara ya Utawala Bora, idara ndani ya ofisi ya rais, ilipewa madaraka ya kutekeleza sheria za kupambana na rushwa, kuratibu jitihada za kupambana na rushwa na kukusanya taarifa kutoka wizara zote kwa kuchapishwa katika ripoti za robo mwaka; hata hivyo, kitengo hiki cha watu watatu kiliendelea kuwa na upungufu mkubwa wa rasilimali.

Kwa upande wa bara TAKUKURU iliwajibika na kuchunguza kesi za rushwa na kuzipeleka mahakamani kwa kuendesha mashtaka. Kwa mfano, Daily News la tarehe 11 Septemba liliripoti kukamatwa na TAKUKURU kwa wabunge wawili na wanachama wengine tisa wa CCM huko Arusha kwa kuwahonga wapiga kura wakati wa Kampeni za viti vya uongozi wa Chama wa mkoa na wilaya. Ukamataji mwingine wa watu kadhaa ulifanyika mkoani Mwanza kwa tuhuma kama hizo za rushwa.

TAKUKURU haifanyi shughuli Zanzibar na inabakia chini ya Mamlaka ya Ofisi ya Rais, mambo ambayo yanazuia uwezo wake wa kuhimili mashinikizo ya kisiasa na kuendesha kesi za ufisadi. TAKUKURU imeendelea kupeleka kesi za rushwa kubwa kwa Mkurugenzi Mwendesha Mashtaka; hata hivyo, mashtaka ya kesi za rushwa yameendelea kuendeshwa taratibu na bila ya ufanisi. Wananchi na vyombo vya habari waliikosoa TAKUKURU kwa kuwashtaki wale wanaojihusisha na rushwa ndogo ndogo.

Kwa mujibu wa TAKUKURU, malalamiko mengi yanayohusiana na rushwa yanahusu serikali kujihusisha katika uchimbaji madini, masuala ya ardhi, nishati na uwekezaji. Kuelekea mwisho wa mwaka, Mkurugenzi Mkuu alieleza kuwa TAKUKURU ilikuwa inachunguza asilimia 20 zaidi ya kesi za rushwa kuliko mwaka uliopita, ikiwa ni pamoja na kesi zinazohusisha tuhuma za rushwa katika sekta ya umma.

AZISE ziliripoti kuwa tuhuma za rushwa zilizo nyingi zilihusisha Mamlaka ya Mapato Tanzania, viongozi wa Serikali za Mitaa, viongozi wanaotoa leseni, wafanyakazi wa hospitali, na vyombo vya habari. Katika mwaka huo, umma ulifahamishwa kuhusu Benki Kuu, Wizara ya Utalii na Wizara ya Fedha.

Mwaka 2006 viongozi huko Zanzibar waliendelea kutokubaliana na jitihada za Serikali ya Muungano za kufungua Ofisi ya Maadili ya Viongozi huko Zanzibar ili kuchunguza rushwa huko. Mwezi Juni, Ofisi ya Zanzibar ya Tuume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilipata idhini kutoka Serikali ya Zanzibar ya kuchunguza matukio yote ya rushwa.

Kupata taarifa za serikali kumebakia kuwa kwa shida sana. Kwa mfano, makala kwenye This Day la tarehe 2 Julai liliripoti matokeo ya utafiti uliofanywa na Haki Elimu, AISE ya nchini na Mradi wa Bajeti wa Kimataifa, AISE ya Kimataifa, ambao ulionyesha kuwa wananchi hawapati taarifa kuhusu shughuli za fedha na bajeti ya serikali. Mabadiliko ya sheria ya mwaka 2005 ya kutoa nafasi kwa wananchi kupata taarifa inavyoonekana hakukubadilisha hali hii – sheria haitaji wazi taarifa za serikali. Viongozi wa Serikali walikadiria kuwa asilimia 90 ya nyaraka zote za serikali, ikiwa ni pamoja na fomu za

utawala, zilichukuliwa kama zilizowekwa katika madaraja. Kwa mujibu wa mawakili wa kupata taarifa, sheria zinazohusiana na usalama wa taifa, utangazaji, magazeti, magereza, maeneo yaliyozuiliwa, siri za viongozi na polisi kuzuia wananchi kupata taarifa za serikali. Hakukuwa na utaratibu wa kuomba kukataa.

Bunge limeendelea kutumia Mfumo wa Bunge wa Taarifa kwenye Mtandao (POLIS) kuongeza upatikanaji wa taarifa za serikali. Hata hivyo, kuipata POLIS bado kumekuwa kwa shida, kwa kuwa ni takriban raia 300,000 kati ya milioni 37 wanapata Intaneti.

**Sehemu ya 4:** Mtazamo wa Serikali kuhusiana na Uchunguzi wa Kimataifa na Usio wa Kiserikali wa Tuhuma za Ukiukaji wa Haki za Binadamu.

Vikundi vingi mbalimbali vya haki za binadamu vya ndani ya nchi na vya kimataifa kwa ujumla viliendeshwa bila vizuizi vya serikali, vikichunguza na kuchapisha matokeo yao kuhusu matukio ya haki za binadamu. Idadi ya AISE iliongezeka haraka katika mwaka, na kwa ujumla viongozi wa serikali walionyesha ushirikiano na kuitikia maoni yao. Kulikuwa na uratibu na ushirikiano mkubwa kati ya serikali ya Zanzibar na AZISE. Serikali ya Zanzibar inazichukulia AZISE kama washirika katika maendeleo, lakini inaendelea kutozivumilia AZISE ambazo zinaikosoa serikali.

Ingawa wabunge wengi hapo zamani walielezea kutoziamini AZISE, mtazamo wao umebadilika sana chini ya utawala wa Rais Kikwete, kwa mujibu wa waangalizi wa kujitegemea. Wabunge wanawake walitambua shughuli za AZISE katika kutoa huduma mbalimbali katika ngazi ya wananchi. Spika mpya wa Bunge la Taifa aliziruhusu AZISE kufika bungeni katika mwaka huo; hata hivyo, ushirikiano kati ya wabunge na AZISE katika utungaji wa sera, ufuatiliaji na tathmini ya sera ya umma ulikuwa bado ni mdogo.

AZISE za nchini za haki za binadamu zilizo hai ni pamoja na Programu ya Mtandao wa Jinsia Tanzania, Haki Elimu, Kituo cha Uendelezaji wa Haki za Binadamu, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania na Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania. Pia kulikuwa na AZISE ndogo za nchini za haki za binadamu ambazo iko nje ya Dar es Salaam. Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar kilikuwa ni kimoja kati ya asasi chache hai za haki za binadamu huko Zanzibar. Asasi zote hizi hazikuitegemea serikali.

Wawakilishi wa serikali walikutana na AZISE za haki za binadamu za nchini na kushiriki katika semina za mafunzo kuhusu mada zilizojumuisha sheria ya kimataifa ya misaada ya hisani, ukeketaji wa wanawake, ajira ya watoto, biashara ya usafirishaji watu na haki za wanawake.

Sheria ya AZISE ya 2002, ambayo haitumiki Zanzibar, inazitaka AZISE zote kujisajili katika kitengo cha kuratibu AZISE kilichoteuliwa na serikali kilicho ndani ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Tangu Februari 2005 hadi Desemba 2006, zaidi ya AZISE 1,000 (baadhi mpya na baadhi zilikuwepo) zilijisajili kwenye kitengo cha uratibu wa AZISE chini ya sheria. Jumla ya AZISE zaidi ya 2,000 ziliandikishwa na kuingia katika Data hazina hadi mwisho wa mwaka.

Kwa upande wa bara, Mwezi Aprili 2006 AISE ya elimu ya Haki Elimu, ambayo ilikuwa imekatazwa na serikali kuchapisha makala au masomo katika shule, na ilizuiwa kuhamasisha na kuwezesha uandishi wa habari wa kuchunguza na kusimamia jamii.

Kulikuwa na kiwango cha kuridhisha cha ushirikiano kati ya serikali na UNHCR, ambao umewezesha kuwepo kwa kiasi kikubwa cha shughuli za kambi 10 za wakimbizi magharibi mwa Tanzania. Katika mwaka huu serikali iliamua kufunga kambi zote za wakimbizi hadi kufikia mwisho wa mwaka. UNHCR ilikubaliana kuongeza muda hadi Juni 2008. Pia serikali kuwapa uraia wa Tanzania wakimbizi zaidi ya 100,000.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inajiendesha yenyewe bila kuingiliwa na serikali. Inapata ushirikiano wa serikali upande wa bara na pia katika mwaka huo ilianza shughuli Zanzibar. Tume iliajiri watu zaidi ya 160 na kuendeshwa kwa kugharimiwa na bajeti ya serikali ya kiasi cha dola milioni 2.27 (shilingi bilioni 2.6). Hata hivyo, ilibakia kupata fedha kidogo, kuwa na wafanyakazi wachache na kuelemewa na wingi wa kesi za malalamiko yasiyotafutiwa ufumbuzi. Bajeti ya tume kwa mwaka 2007 – 08 ilipunguzwa kwa asilimia 13 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2006-07. Tume ilipokea ongezeko la idadi ya malalamiko kutokana na kampeni za uelimishaji zilizoendeshwa kupitia vyombo vya habari. Kuanzia Juni 2006 hadi Juni 2007, tume ilipokea jumla ya malalamiko mapya 4,948 kuhusu masuala ya haki za binadamu na haki ya kiutawala, ongezeko la karibu asilimia 30 ukilinganisha na mwaka uliopita. Mwishoni mwa mwaka maktaba ya tume ilitoa data hazina zilizohifadhiwa katika kompyuta kwenye mtandao, lakini mfumo wa usimamizi wa kesi na utunzaji wa kumbukumbu ulikuwa bado ukifanywa kwa kuandika kwa mkono.

Kamati ya Katiba, Sheria na Uongozi wa Umma ya Bunge la Muungano inawajibika kuripoti na kutoa mapendekezo kuhusiana na haki za binadamu. Ingawa wajumbe wa kamati walio wengi walikuwa wanatoka chama tawala cha CCM, hata hivyo, kamati ilifanya kazi bila ya kutegemea ushawishi wa serikali na chama tawala na watazamaji wengi waliiona kama asasi isiyo na upendeleo.

Serikali imeendelea kuwa mwenyeji wa Mahakama ya Kimataifa ya Mauaji ya Rwanda (ICTR) iliyoko Arusha, na serikali iliendelea kutoa msaada na kushirikiana na ICTR.

**Sehemu ya 5:** Ubaguzi, Unyanyasaji wa Kijamii na Biashara ya Kusafirisha Watu

Katiba inakataza ubaguzi unaohusisha utaifa, kabila, ushiriki katika siasa, rangi au dini; hata hivyo, serikali wakati wote haitekelezi ipasavyo kukataza huko. Ubaguzi unaohusisha jinsia, umri au ulemavu haukukatazwa kwa uwazi na sheria bali unazuiwa hadharani katika kauli za viongozi na sera za serikali. Ubaguzi dhidi ya wanawake, wakimbizi, walio wachache na watu wenye VVU/UKIMWI uliendelea, na wasiwasi wa makabila ya jamii uliendelea kuwa tatizo katika baadhi ya maeneo ya nchi.

**Wanawake**

Sheria inataja kifungo cha maisha kwa watu wanaotiwa hatiani kwa kubaka; hata hivyo, ubakaji umeendelea kuwa tatizo kubwa. Katika mwaka huo watu kadhaa walishtakiwa na kutiwa hatiani kwa kubaka na kushambulia chini ya sheria. Inakadiriwa asilimia 5 tu ya kesi za kubaka zilipelekwa mahakamani kwa mashtaka. Mwezi Agosti, Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake kiliandaa mkutano ambapo iliripotiwa kwamba inakadiriwa asilimia 80 ya waathirika wa ubakaji hawakuripoti matukio yao.

Kwa mujibu wa Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, wakati mwingine kesi zinafutwa kutokana na kukosa ushahidi. Iliripotiwa kuwa baadhi ya polisi waliwashauri waliobakwa kunawa kabla ya kwenda hospitali kwa uchunguzi, na kusababisha kupotezwa kwa ushahidi muhimu. Mwaka 2006, kisiwa kikuu cha Zanzibar, Unguja, kilikuwa na hospitali moja tu ya binafsi ambayo ilifanya uchunguzi wa baada ya kubakwa, lakini sheria inataka uchunguzi baada ya kubakwa ufanyike katika hospitali ya serikali. Kwa kuongeza, kwa kuwa wanaobakwa inabidi wasubiri siku hadi sita kwa ajili ya uchunguzi, ushahidi mkubwa muhimu ulipotea. Hospitali pekee ya serikali katika kisiwa cha Pemba inafanya uchunguzi baada ya kubakwa mara moja tu kwa wiki.

Ubakaji na unyanyasaji kingono wa wasichana na wanawake walemavu ulioripotiwa ulienea katika mwaka huo. Utumiaji nguvu wa kingono na uliohusisha jinsia uliendelea kuwa tatizo katika kambi za wakimbizi. Utumiaji nguvu majumbani dhidi ya wanawake uliendelea kuenea sana. Sheria inakataza kushambulia lakini haikatazi wazi kumpiga mke/mume. Shughuli nyingi za kiutamaduni; kifamilia na kijamii mara nyingi zinawazuia wanawake kutoa ripoti za kunyanyaswa, na mara chache viongozi wanachukua hatua dhidi ya unyanyasaji wa kimwili wa wanawake. Kama ilivyokuwa kwa miaka iliyopita, polisi waliripotiwa mara nyingi kukataa kushughulikia kesi za unyanyasaji majumbani.

Mwezi Aprili 2006 utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani uliripoti kuwa takriban asilimia 25 ya wanawake waliohojiwa waliripoti kuwa walikumbana na utumiaji nguvu wa kimwili na kingono kutoka kwa wasio wenzi wao tangu wakiwa na miaka 15. kiasi cha moja ya 10 waliripoti unyanyasaji kingono kabla ya umri wa miaka 15.

Mahakama zinatambua utumiaji nguvu majumbani kama sababu za talaka. Hata hivyo, mara nyingi wanawake walivumilia unyanyasaji wa nyumbani kwa muda mrefu kabla ya kuomba talaka; wale walioomba ushauri kutoka kliniki za msaada wa kisheria bara walio wengi walitaja unyanyasaji wa majumbani kama sababu ya kutaka talaka. Hata hivyo, kihistoria jamii inachukulia upigaji wa mke kuwa kitendo kinachokubalika, na wakati mwingine wanawake waliadhibiwa na waume zao kwa kutozaa watoto.

Sheria inakataza ukeketaji wa wanawake, pia unajulikana kama tohara ya wanawake; hata hivyo, ulikuwa ukifanywa na makabila na familia nyingi, na wale waliofanya shughuli hiyo mara chache sana waliwajibishwa. Adhabu za kufanya ukeketaji kwa wanawake chini ya miaka 18 zilikuwa kifungo cha kuanzia miaka mitano hadi 15, faini isiyozidi dola 235 (shilingi 300,000), au vyote. Pia sheria inaeleza malipo ya fidia anayotoa mkosaji kwa mtu aliyetendewa kosa. Sheria haitaji kiwango cha chini cha faini

na haielezi ulinzi wa kisheria kwa wanawake wenye miaka 18 au wakubwa zaidi. Sheria inaeleza kwamba mtu yeyote anamlea, anamsimamia au kumtunza msichana wa miaka chini ya 18 na ambaye anamsababishia kukeketwa, anatenda kosa la ukatili kwa watoto.

Ripoti ya Wizara ya Afya iliyotolewa mwezi Desemba, 2006 ilionyesha kuwa asilimia ya wanawake na wasichana wanaokeketwa ilipungua kutoka asilimia 18 mwaka 1995 hadi asilimia 15 mwaka 2005. Takwimu nyingine zinaonyesha kuwa wastani wa umri wa waathirika umepungua hadi chini ya miaka 10, pamoja na watoto wanaozaliwa walioripotiwa kufanyiwa ukeketaji. Katika mkoa wa Singida, ukeketaji wanawake mara nyingi ulifanywa kwa watoto wachanga walipougua malaria au magonjwa mengine ili athari zozote zenye madhara zinazotokana na kitendo hicho zisisababishe mashaka miongoni mwa majirani na ndugu. Ukeketaji wa wanawake ulifanywa na takriban makabila 20 kati ya 130 ya nchini na ulienea sana katika mikoa 11 ya bara, ikiwa ni pamoja na Arusha, Singida, Kilimanjaro, Morogoro na Dar es Salaam. Katika maeneo mengine ya nchi, asilimia chini ya 5 ya watu wanafanya ukeketaji wa wanawake. Ukeketaji uliofanyika sana ulikuwa wa ukataji wa kinembe, aina ya ukeketaji isiyo mbaya sana; hata hivyo ukataji kinembe na kushona sehemu za siri ni aina mbaya sana, pia ilifanywa hasa nyanda za juu kaskazini na kanda ya kati.

Tarehe 20 Oktoba, kulikuwa na ripoti kwamba msichana wa miaka sita alitokwa damu hadi kufa baada ya kufanyiwa tohara katika wilaya ya Iramba, mkoa wa Singida. Mama wa mtoto na Mtuhumiwa mwingine mmoja walikuwa wanashikiliwa na Polisi. “Ngariba,” aliyemfanyia mtoto kitendo hicho alikuwa bado hajapatikana.

Hapakuwa na ripoti za mashtaka yanayohusiana na ukeketaji wa wanawake katika mwaka huo. Utekelezaji wa sheria ya kupambana na ukeketaji wa wanawake ulikuwa mgumu kutokana na sababu kadhaa: maofisa wengi wa polisi na jamii nyingi hazikuifahamu sheria; polisi hawakuwa na rasilimali za kutosha kuwalinda waathirika; na mara nyingi waathirika walikataa kutoa ushahidi dhidi ya wanafamilia au majirani ambao waliwalazimisha kufanyiwa ukeketaji. Baadhi ya mashahidi waliogopa visasi kutoka kwa wanaounga mkono ukeketaji.

Pia rushwa imefanya kuwa vigumu kutekeleza sheria ya kupambana na ukeketaji. Baadhi ya wanavijiji waliripotiwa kuwapa viongozi wa maeneo kiasi kikubwa cha dola 235 (shilingi 300,000) ili waruhusiwe kuwafanyia tohara mabinti zao bila ya kuogopa kukamatwa au kushtakiwa.

Serikali iliendeleza kutekeleza mpango wa taifa wa utekelezaji wa 2001-15 wa uzuiaji na ukomeshaji wa utumiaji nguvu dhidi ya wanawake na watoto. Mkakati huu, uliojumuishwa kama dhamira ya maadhimisho ya mwezi Machi ya Siku ya Wanawake Duniani, ukijaribu kukomesha kabisa ukeketaji kwa kuwahusisha waganga na viongozi wa jamii, na wanawake na wanaume. Vikundi vya kupambana na ukeketaji viliwaomba wabunge na viongozi wa Serikali za Mitaa kuchukua jukumu kubwa katika kutekeleza sheria, ingawa wabunge hawana mamlaka ya kutekeleza sheria.

Katika mwaka huo serikali na AZISE walipiga hatua katika kupunguza shughuli ya wazi ya ukeketaji wanawake. Mtandao wa Kupambana na Ukeketaji wa Wanawake na

Muungano wa AZISE Zinazopambana na Ukeketaji walijihusisha katika shughuli za uelimishaji na kuendesha utafiti kuhusu ukeketaji. Vikundi vya kupambana na ukeketaji viliendelea kuwaelimisha mangariba kuhusu athari mbaya za ukeketaji na kuwapa mafunzo ya kazi nyingine. AISE ya TAMWA ilisisitiza kwamba kupitishwa kwa sheria mwaka 1998 bila ya kutoa mafunzo kwa maofisa wa polisi kulikuwa hakutoshi kupambana na mila na desturi.

Kupunguza shughuli ya ukeketaji ilibakia kuwa vigumu kwa sababu baadhi ya viongozi wa serikali wa mkoa walipendelea au kufaidika na shughuli hiyo au walihofia kuzungumzia kupingana nayo kwa sababu ya kuogopa matokeo ya kisiasa ya kupinga ukeketaji na nguvu ya viongozi wa kimila ambao wanaunga mkono ukeketaji. Baadhi ya jamii ambazo ziliifahamu sheria inayokataza ukeketaji ziliiona kama kitisho kisicho cha haki kwa mila na utamaduni. Ukosefu wa taarifa za kitabibu kuhusu madhara na athari za kiafya za muda mrefu za ukeketaji limebakia kuwa tatizo. Jamii nyingi zinaamini ukeketaji unaongeza uzazi, unapunguza hamu ya kufanya ngono inayosababisha ukahaba na kupunguza vifo vya watoto. Akina baba wengi waliamini wangepata mahari kubwa kwa mabinti ambao wamekeketwa. Aidha, mangariba wanaitegemea shughuli hii kwa kipato.

Sheria inakataza ukahaba; hata hivyo, ukahaba umeendelea kufanywa. Mara kadhaa makahaba wanakamatwa lakini polisi hawaweki takwimu rasmi za idadi au mpangilio wa kesi. Wanawake na wasichana maskini wa vijijini wanaohamia maeneo ya mijini wengi wao walikuwa hatarini.

Sheria inakataza unyanyasaji wa kijinsia wa wanawake mahali pa kazi. Ukubwa wa tatizo haukujulikana.

Sheria ya urithi na ndoa haitoi usawa kamili kwa wanawake, na katika utekelezaji mara nyingi haki za wanawake haziheshimiwi. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto, na Wizara ya Sheria ziliwajibika kulinda haki za kisheria za wanawake. Ubaguzi dhidi ya wanawake ulikuwa mkubwa sana maeneo ya vijijini ambako wanawake walifanya kazi ya kulima na kulea watoto. Wanawake wa vijijini wamekuwa na fursa ndogo ya kwenda shule au kupata ajira ya malipo.

Katika masuala ya familia, maudhui na matumizi ya baadhi ya sheria za kimila na za Kiislamu zina ubaguzi dhidi ya wanawake, kote bara na Zanzibar.

Sheria ya nchi ya uhamiaji haitambui kwamba mwanamume anaweza kuwa mtegemezi, na kufanya kuwa vigumu kwa mwanamume mgeni ambaye ni mume wa mwanamke raia kupata kibali cha makazi. Kwa kuwa serikali haitambui uraia wa sehemu mbili, mwanamke raia aliyeolewa na mwanamume ngeni inaweza kuwa vigumu kuishi kihalali nchini, na katika utekelezaji, anaweza kulazimishwa kuukana uraia wake. Hili limezidi kuwa tatizo katika kambi za wakimbizi kwa wanawake wa Kitanzania ambao wameolewa na wanaume Warundi ambao hawastahili kupata kibali cha ukazi kwa sababu ya hadhi yao ya ukimbizi.

Sheria inawapa watu haki ya kutumia, kuhamisha na kumiliki ardhi bila ya kutofautisha jinsia, na inatambua haki za umiliki za wanawake. Wahamasishaji wa vyama vya kiraia waliripotiwa kueneza ubaguzi dhidi ya wanawake katika masuala ya mali yanayohusiana na urithi na talaka. Hii hasa ilitokea Zanzibar na sehemu za bara ambako mahakimu walifanya makubaliano na sheria ya mila na ya Kiislamu. Wanawake ambao kuolewa kwao kulikuwa hakujahalalishwa chini ya sheria za kimila, Kihindu, Kiislamu, Kikristo au kiserikali waliathirika kama walitengana na waume zao au waume zao walifariki.

Huko Zanzibar, wanawake wanaopata mimba nje ya ndoa wanaweza kushtakiwa na kuhukumiwa kufanya kazi za kijamii kwa kosa hilo; Ofisi ya Mkurugenzi Zanzibar ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali ilichapisha kanuni ambazo zinataja aina ya huduma ya kijamii ambayo inaweza kutolewa.

**Watoto**

Serikali iliendelea kujihusisha na haki na ustawi wa watoto. Serikali ilifanya jitihada zenye kusaidia kushughulikia ustawi wa watoto, ikiwa ni pamoja na ushirikiano wa karibu na asasi za kimataifa na za nchini ili kuboresha hali njema ya watoto waliotelekezwa na watoto yatima nchini wanaokadiriwa kuwa milioni 2.5

Sheria inaeleza kuwa elimu ya lazima ni miaka saba hadi umri wa miaka 15 kwa watoto wote. Elimu ya msingi ilikuwa ni ya lazima, bure na kwa wote bara na Zanzibar; hata hivyo, kulikuwa na idadi isiyotosheleza ya shule, walimu, vitabu na vifaa vingine vya elimu kukidhi mahitaji.

Katika mwaka huo ada iliendelea kutozwa kwa uandikishaji unaozidi kidato cha pili, sawa sawa na mwaka wa pili wa kidato cha tano na sita. Matokeo yake, baadhi ya watoto hawakupata nafasi ya kusoma elimu ya sekondari; hata hivyo, mwaka 2005 serikali ilipunguza ada ya shule kwa nusu na kutoa ruzuku kufidia ada zilizobakia kupitia programu ya maendeleo ya shule za sekondari. Ada ya wanafunzi wa kutwa ilikuwa dola 15 (shilingi 20,000) na ada ya shule ya bweni dola 61 (shilingi 80,000) kwa mwaka. Aidha, wazazi wengi ilibidi walipie vitabu, sare za shule na chakula cha mchana shuleni.

Viwango vya jumla vya kumaliza shule vilikuwa sawa kwa wavulana na wasichana; asilimia 56 kwa shule ya msingi na asilimia 33 kwa sekondari.

Ubakaji wa watoto liliendelea kuwa tatizo, na kulikuwa na mashtaka katika mwaka huo; watu wengi walioshtakiwa kwa ubakaji wa watoto walihukumiwa kifungo cha juu cha miaka 30 gerezani.

Adhabu ya kupiga mashuleni lilikuwa ni tatizo. Viboko viliruhusiwa na sheria, ingawa kitendo hicho kiliendelea kupungua katika mwaka kufuatia jitihada za serikali kuwafikia wananchi wote, hasa Wizara ya Elimu na Vyombo vya habari. Mwezi Oktoba mtoto wa shule ya kati katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Maswa aliumizwa vibaya kutokana na kuchapwa viboko na makamu wa mkuu wa shule.

Chini ya sheria, kufanya ngono na mtoto chini ya miaka 18 kunachukuliwa kama kubaka bila ya kujali ridhaa; hata hivyo; sheria ilikuwa haitekelezwi ipasavyo. Katika tofauti

zilizo wazi, sheria ya familia inaeleza wasichana wadogo wa miaka 15 kuchukuliwa kama watu wazima kwa madhumuni ya kuolewa na kujamiiana. Ili kuolewa, msichana chini ya miaka 18 anatakiwa kupata ridhaa ya baba yake, mama au mlezi. Msichana yatima asiye na mlezi ambaye anataka kuolewa katika umri wa miaka 15, 16 au 17 hahitaji ridhaa. Mahakama zina uamuzi wa kuruhusu ndoa za watu wenye miaka 14 kama wanaridhika kwamba kulikuwa na mazingira maalumu ambayo yanafanya ndoa iliyopendekezwa kufaa. Kwa kuongeza, sheria inawaruhusu wasichana Waafrika wenye asili ya Kiasia kuolewa wadogo wakiwa na miaka 12 ili mradi ndoa itakamilishwa kwa kufanya ngono hadi msichana atakapofikisha miaka 15.

Katika mwaka serikali iliendeleza jitihada zake za kutekeleza sheria inayomuadhibu mtu yeyote anayehusika na kumpa mimba msichana wa shule. Mwezi Aprili mwalimu wa shule ya msingi ya Kibuye, Suzi Bosobi, alikamatwa kwa tuhuma za kumpa mimba mwanafunzi mwenye umri wa miaka 14 ambaye alijifungua na kumtupa mtoto kwenye choo cha shimo. Mtoto aliokolewa lakini alifariki baada ya muda mfupi.

Tarehe 26 Septemba, mwalimu mkuu wa shule ya msingi ya Ikungumhulu katika Wilaya ya Misungwi, mkoa wa Mwanza alishtakiwa kwa kumbaka mwanafunzi mwenye miaka 16. Alikana mashtaka na kaachiwa kwa dhamana.

Sheria inataja ukahaba wa watoto kuwa ni uhalifu; hata hivyo, unyonyaji wa kingono na biashara ya usafirishaji watu, ikiwa ni pamoja na watoto, yalikuwa ni matatizo.

Kulikuwa na ripoti mbalimbali kwamba watu wanaofanya uchawi wanaua watoto; walituhumiwa kuondoa na kuuza viungo vya mwili na ngozi. Mauaji ya watoto wadogo wa kiume na wa kike liliendelea kuwa tatizo. Mwezi Juni 2006, miili 22 ya watoto wachanga ilikutwa katika maeneo ya kutupia takataka huko Arusha. Polisi aliyefanya uchunguzi wa maiti aliripoti kuwa watoto walikufa kwa kukosa hewa. Hadi mwisho wa mwaka hapakuwa na ripoti ya mashtaka kwa kosa hili. Kesi za kutupa watoto ziliendelea kuripotiwa katika mwaka huo.

Idadi ya yatima nchini ilikadiriwa kuwa zaidi ya milioni mbili, wengi wao wamekuwa yatima kutokana na UKIMWI. Kwa ujumla yatima walichukuliwa kwenye familia nyingine, wale ambao hawakuchukuliwa walionekana kama watu walio katika hatari kubwa na walipata msaada wa ziada na unasihi. Kulikuwa na idadi kubwa ya watoto wa mtaani katika Miji ya Dar es Salaam na Arusha. Watoto wa mtaani walikuwa na nafasi ndogo ya kupata huduma za afya na elimu kwa sababu hawana makazi ya kudumu na fedha za kununua dawa, sare za shule na vitabu. Pia walikuwa hatarini kubakwa na watoto wa mtaani wakubwa na watu wasio na makwao.

**Usafirishaji watu**

Sheria haikatazi aina zote za biashara. Tanzania ni nchi ya chanzo, kupitisha na mwisho wa safari kwa wanawake na wasichana wanaosafirishwa kwa ajili ya kazi ya kulazimishwa na unyonyaji kingono na kwa kiasi kidogo, wavulana wanasafirishwa kwa kazi ya kulazimishwa.

Ilikuwa haiwezekani kutathmini tukio la usafirishaji watu katika mwaka, lakini tukio limekuwepo katika mikoa mingi nchini. Waathirika wengi walisafirishwa ndani ya nchi; wavulana walisafirishwa kwa kazi za unyonyaji katika mashamba, kwenye madini na katika sekta kubwa isiyo rasmi wakati wasichana kutoka maeneo ya vijijini walisafirishwa kwenda mijini kwa kufanya kazi za ndani kwa hiari. Baadhi ya vijana hawa wanawatoroka waajiri wanyanyasaji na kuwa makahaba ili waweze kuishi. Waathirika wengi walitokea mikoa ya Iringa, Mwanza, Dododma, Kigoma, Dar es Salaam na Arusha. Idadi ndogo ya watu waliripotiwa kusafirishwa kwenda Afrika Kusini, Saudi Arabia, Uingereza, na pengine nchi nyingine za ulaya kwa ajili ya utumwa wa majumbani. Wanawake wa kihindi – ambao waliingia nchini isivyo halali kufanya kazi kama wanamuziki, waimbaji na wacheza dansi katika migahawa na klabu za usiku – wakati fulani walinyonywa kama makahaba baada ya kuwasili. Huko Zanzibar baadhi ya hoteli zinawafadhili wasichana kwa kazi za hoteli ambao baadaye wanakuwa wahudumu wa baa au makahaba; hoteli zilitumiwa na wasafirishaji watu kwa shughuli za ukahaba.

Kuanzia Septemba, Ofisi ya Kimataifa ya Uhamiaji (IOM) ilizindua kampeni ya kuwaelimisha watu kuhusu tatizo la usafirishaji watu nchini Tanzania na kuhamasiaha mjadala wa umma wa suala hilo na viongozi wa taifa na wanaotoa maoni. IOM ilirusha hewani kipindi cha kuonyesha hali halisi na kutayarisha na kusambaza makala na matangazo katika televisheni kuhusu kusafirisha watu.

Katika mwaka huo, AISE ya KIWOHEDE na Watoto katika Jua waliwasaidia waathirika 76 wa biashara ya usafirishaji watu na kuwapima afya waathirika 120. Aidha, waathirika 120 walipelekwa shule au kupata mafunzo ya ufundi stadi na watoto 91 waliunganishwa tena na familia zao. Baadhi ya waathirika waliookolewa walipewa msaada wa fedha za shule au miradi midogo ya kuzalisha kipato.

Watoto walio katika familia zenye kipato kidogo walikuwa katika hatari kubwa ya kusafirishwa kwa biashara, na watoto walikuwa hatarini zaidi kuliko wavulana kwa kuwa walichukuliwa kama mzigo wa kiuchumi zaidi katika familia zao. Pia nchi ilipata ongezeko kubwa katika idadi ya watoto wanaoongoza familia kwa kuwa watu wazima wengi walikumbwa na ugonjwa na vifo vinavyohusiana na VVU/UKIMWI, na kuwaacha wategemezi wao katika hatari kubwa ya ajira ya watoto na usafirishaji wa watu.

Njia za usafirishaji watu zinatofautiana. Waathirika walishawishiwa na ahadi ya kipato, fursa ya kwenda shule, na hali bora ya maisha, hasa kutoka maeneo ya vijijini kwenda mjini. Baadhi ya waathirika wa kusafirishwa huonekana majumbani kwao kwa msaada wa familia zao; baadhi huondoka wenyewe kukimbia maisha katika maeneo ya vijijini; na baadhi walisafirishwa na mtu aliyewaahidi kupata kazi jijini, kihalali au vinginevyo. Kulikuwa na ripoti kwamba wanaume waliwaajiri wasichana wa kijijini waliomaliza elimu ya msingi lakini hawakuendelea sekondari. Wanaume waliwapa wasichana fedha na ajira na kuwaahidi wasichana maisha mazuri kama wataenda nao mjini. Njia nyingine ya usafiirshaji watu ilihusisha wazazi wenye kipato kidogo wanaomkabidhi mtoto kwa ndugu wenye uwezo au mwanajamii anayeheshimiwa, ambao walikabidhiwa mtoto wamlee kama mmoja wa watoto wao. Baadhi ya watu waliitumia nafasi hiyo ya taratibu za kimila na kumuweka mtoto katika mazingira ambayo alikuwa katika hatari ya kunyonywa na kunyanyaswa. Wakati fulani mawakala wa shughuli ndogondogo, wa

kujitegemea waliajiri watoto kutoka vijijini na kuandaa mipango na usafiri hadi kwenye familia.

Hapakuwa na mashtaka ya usafirishaji watu katika mwaka kwa kuwa nchi haikuwa nasheria mahususi ya usafirishaji watu; hata hivyo, wakosaji walishtakiwa chini ya vifungu vingine vya sheria, kama vile kwa kubaka.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, pamoja na ushirikiano kutoka nje, iliandaa kitabu cha mwongozo wa mafunzo kwa wafanyakazi wa afya ambao wanakutana na waathirika wa usafirishaji watu. Tarehe 19 Juni, wizara iliendesha mafunzo kwa wafanyakazi wa afya 300.

Kulikuwa na ripoti zilizotengwa kuwa viongozi wa polisi walipokea rushwa ili kupuuzia unyonyaji wa biashara ya ngono.

Serikali ilishirikiana na AZISE na kuisifia kazi ya IOM. Katika mwaka KIWOHEDE na Watoto katika Jua walipata mafunzo kuhusu kutambua na kuwasaidia waathirika iliyoandaliwa na IOM. Kati yao waliwaondoa wavulana 12 na wasichana 28 kutoka mazingira ya ajira ya watoto; wasichana 20 kati ya 28 waliosaidiwa hawakuwahi kusoma shule yoyote. Wasichana walikuwa wakielekezwa kwenye AZISE wakati wavulana walienda wenyewe katika makazi ya AZISE. Waathirika wote wanaosaidiwa na IOM walipata huduma za upimaji wa afya, unasihi wa kisaikolojia, makazi, nguo, kuongeza ujuzi, na pale ilipowezekana, uunganishwaji na familia pamoja na msaada wa fedha za kuanzisha biashara ndogo (wakati msichana anapopata mafunzo ya ufundi stadi) na msaada wa familia. Waathirika kumi na wawili waliunganishwa na familia zao katika mwaka.

**Watu wenye Ulemavu**

Katiba inakataza ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu; lakini hakuna sheria maalumu ya kutekeleza sharti hili. Watu wenye ulemavu wa viungo hawakupata nafasi katika ajira, elimu, kupata huduma ya afya na huduma nyingine za taifa kwa vikwazo vya maumbile na rasilimali isiyotosheleza ya bajeti. Serikali imeagiza watu wenye ulemavu kuwezeshwa kufika kwenye majengo ya umma, usafiri au kupata huduma za serikali kupitia vifungu kadhaa vya sheria, kama vile sheria ambayo inazuia utoaji wa vibali vya ujenzi kwa majengo ambayo hayatoi nafasi kwa watu wenye ulemavu. Hata hivyo, majengo machache yaliweza kufikika, si majengo yote yanahitaji vibali vya ujenzi, na majengo yaliyo mengi nchini yalijengwa kabla ya 1997, wakati sharti hili lilipoanza kutekelezwa. Hakuna fedha zilizotolewa kwa ajili ya kurekebisha majengo yaliyopo.

Wizara za Elimu, Sheria na Kazi ziliwajibika na kutekeleza ulinzi dhidi ya haki za watu wenye ulemavu kwa ajili ya elimu, madai ya kisheria na haki za kazi. Idara ya Ustawi wa Jamii ilikuwa na jukumu la kuratibu masuala ya ulemavu. AZISE chache za nchini zilijaribu kusisitiza hali halisi katika jamii ya watu wenye ulemavu.

Katika mwaka husika Wizara ya Elimu iliendelea kusaidia mfuko maalumu ulioanzishwa ili kuongeza upataji elimu, hususan wa watu wenye ulemavu na wanajamii wengine

wenye matatizo. Fedha zilitumika kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu kuendelea na masomo yao baada ya kufaulu mitihani ya darasa la saba nchini.

Kulikuwa na ripoti mbalimbali kwamba wanafunzi wenye ulemavu waliacha kwenda shule ambazo hazikuwa na vifaa vya kutosha. Kwa mfano karatasi za gharama za Breli na tepurekoda havikuwepo kwa wanafunzi wasioona.

Mwanzoni mwa mwaka serikali iliondoa kizuizi kilichowekwa mwaka 2005 ambacho kiliikataza AISE ya Haki Elimu kushughulikia au kuchapisha utafiti kuhusiana na shule za serikali; hata hivyo; ilibidi AISE ikubali kutoripoti kuhusu mambo ya elimu kwa siku zijazo. Katika tangazo la televisheni la kuikosoa serikali, Haki Elimu ilisisitiza ukweli kwamba shule za serikali hazina vifaa vinavyofaa kwa wanafunzi wasioona na wanafunzi wasio na viungo.

**Taifa/Rangi/Makabila ya walio wachache**

Hapakuwa na sheria au sera rasmi ambazo ziliwabagua Waasia au taifa jingine lolote.

Kulikuwa na matukio ya kipekee ya migogoro ya kikabila kuhusu ardhi na mifugo. Mwezi Septemba uliripotiwa ugomvi kutokea kati ya wafugaji na wakulima huko Mbarali ambao ulisababisha kifo cha mtu mmoja na 12 kujeruhiwa.

**Wenyeji Asilia**

Wabarbaig na makundi mengine ya watu wanaohamahama huko kaskazini waliendelea kutafuta fidia kwa kubaguliwa na serikali siku za nyuma, ambako kunajumuisha jitihada za serikali kuwafanya wafuate mtindo wa maisha wa kisasa na kuwazuia kufika katika ardhi ya kufugia ambayo iligeuzwa kuwa mashamba makubwa ya ngano ya serikali. Viongozi walitoa fidia kwa wenyeji asilia waliohamishwa, lakini matatizo yaliendelea.

Katika mwaka husika iliripotiwa kwamba Wahadzabe, wenyeji asilia wa kaskazini mwa Tanzania, ambao pia wanaitwa watu wa porini, walikabiliana na tishio kubwa la maisha yao. Maeneo yao ya kuwindia na kukusanya chakula yalichukuliwa na waandaaji maarufu wa safari kutoka Jamhuri ya Falme za Kiarabu, ambao walikuwa wanategemea msaada wa Serikali ya Tanzania kuwaondoa Wahadzabe katika eneo.; hapakuwa na ripoti kuwa serikali iliwasiliana na wawakilishi wa Wahadzabe katika kuzingatia jinsi ya kushughulikia jambo hilo.

**Unyanyasaji mwingine wa Kijamii na Ubaguzi**

Usenge na usagaji ni kinyume cha sheria nchini. Sheria huko Zanzibar imeweka adhabu ya kifungo cha hadi miaka 25 kwa wanaume wanaojihusisha na uhusiano wa kisenge na miaka saba kwa wanawake walio katika uhusiano wa kiusagaji. Hapakuwa na ripoti yoyote kwamba mtu yeyote aliadhibiwa chini ya sheria katika mwaka huo.

Muungano wa Wabunge wa Tanzania Wanaopambana na UKIMWI ulishughulikia ubaguzi dhidi ya watu walioambukizwa VVU/UKIMWI. Hata hivyo, kulikuwa na ripoti mbalimbali kwamba ubaguzi majumbani, katika huduma za afya na elimu uliendelea

kutokea dhidi ya watu wanaokadiriwa kuwa milioni 3.5 nchini wanaoishi na VVU/UKIMWI. Kulikuwa na ripoti tofauti kwamba waajiri binafsi waliwafukuza au hawakuwaajiri watu waliofahamika kuwa wana VVU/UKIMWI. Serikali kwa kushirikiana na AZISE inaendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu ubaguzi unaohusiana na VVU/UKIMWI na kutoa ulinzi kwa haki za binadamu za wagonjwa wa VVU/UKIMWI. Rais Kikwete, mke wake na viongozi wa juu serikalini walitangaza kwamba wamepima VVU/UKIMWI. Mtandao wa wanasheria, watunga sera na madaktari wameendelea na jitihada za kushawishi na shughuli nyingine za kushughulikia tatizo la kisheria, kimaadili na haki za binadamu linalohusishwa na VVU/UKIMWI.

**Sehemu ya 6:** Haki za Wafanyakazi

**a. Haki ya Kujumuika**

Sheria inawaruhusu wafanyakazi kuunda au kujiunga na vyama bila ya kuomba idhini kwanza; hata hivyo, katika utekelezaji; waajiri wengi wa sekta binafsi wanafuata sera za kuzuia vyama au mbinu ambazo zinazuia haki hii.

Sheria mpya ya kazi ilianza kutumika mwezi Desemba 2006, ambayo ilianzisha Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii, Tume ya Usuluhishi na Upatanishi na Mahakama ya Kazi; ilitekeleza kanuni na asasi zilikuwa bado zinaanzishwa. Sheria mpya, ambazo zinatumika bara lakini si Zanzibar, zinatambua haki za asasi za vyama vya wafanyakazi na kuanzisha utaratibu wa usajili wa vyama vya wafanyakazi na vyama vya waajiri. Chama cha wafanyakazi ambacho kimesaini zaidi ya asilimia 50 ya sehemu ya mapatano ya pamoja tu ndicho kinaweza kupatana na mwajiri. Chama cha wafanyakazi ama chama cha waajiri lazima kisajiliwe ndani ya miezi sita tangu kuanzishwa; kushindwa kujiandikisha ni kosa la jinai.

Serikali ya Muungano na ya Zanzibar hazina sheria za kazi zinazofanana, na zinatekeleza sheria zao tofauti. Sheria ya kazi ya bara inatumika kwa wafanyakazi wa serikali na wa binafsi. Sheria ya bara inakitaka chama cha wafanyakazi kwa ajili ya waajiriwa kiwe na wanachama angalau 20.

Takriban asilimia 20 ya wafanyakazi ambao walijiunga na ajira ya "sekta rasmi" waliandikishwa katika chama. Shirikisho la vyama vyote, Muungano wa Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), ulikuwa na wanachama 317,000 mwaka 2005 (data za hivi karibuni), au chini ya asilimia 2 ya wafanyakazi wote. Katika sekta ya kilimo ambayo ilikuwa mwajiri mkubwa pekee nchini; inakadiriwa asilimia 5 hadi 8 ya wafanyakazi walijiunga katika chama cha wafanyakazi.

Chini ya sheria, chama cha wafanyakazi kilichosajiliwa bara kinastahili idadi ya wawakilishi katika TUCTA kutegemeana na idadi ya wanachama wake. Kwa mashirika yenye wafanyakazi 100 au zaidi, idadi maalumu ya wawakilishi, inayozingatia wingi wa wanachama, lazima wawe wanawake kama wanawake wameajiriwa katika kitengo.

Kwa upande wa bara sheria inakataza shughuli za ubaguzi kufanywa na mwajiri dhidi ya wanachama wa chama; hata hivyo, kulikuwa na ripoti kadhaa za ubaguzi wa kupingana

na chama katika sekta rasmi binafsi katika mwaka. Waajiri waliopatikana na kosa la kufanya shughuli za kupinga chama, sheria iliwataka kuwarejesha wafanyakazi.

Vyama vingi vya wafanyakazi viliripori kuwa waajiri wa sekta binafsi, hasa wale waliovutiwa nchini kwa ubinafsishaji na marekebisho ya uchumi, walivibagua vyama vya wafanyakazi. Ingawa sheria inakataza vitendo hivyo, baadhi ya wawekezaji hao waliripotiwa kutishia kuwasimamisha au kuwafukuza kazi wafanyakazi waliotaka kujiunga na vyama vya wafanyakazi na baadhi ya waajiri hawakuviruhusu vyama kuitisha na kufanya mikutano ya kuandikisha katika mahali pao pa kazi.

Sheria ya Kazi huko Zanzibar inatumika kwa wafanyakazi wa sekta binafsi tu. Wafanyakazi wa Zanzibar hawakuruhusiwa kujiunga na vyama vya wafanyakazi vya bara. Sheria ya Kazi ya Zanzibar inakitaka chama chenye wanachama 50 au zaidi kuandikishwa na kuweka viwango vya elimu kwa maofisa wa chama cha wafanyakazi.

**b. Haki ya Kuandaa na Kujadiliana Malipo kwa Pamoja**

Sheria inaeleza kujadiliana kwa pamoja katika sekta binafsi, na wafanyakazi na waajiri walifanya hivyo kwa uhuru katika mwaka huo. Katika sekta ya umma, serikali inapanga mishahara kiutawala, ikiwa ni pamoja na ya wafanyakazi wa mashirika yanayomilikiwa na serikali.

Huko Zanzibar sheria inakataza migomo. Kwa upande wa bara, wafanyakazi wana haki ya kisheria ya kugoma na kila mwajiri ana haki ya kuwazuia wasiingie kazini baada ya kufuata masharti na taratibu kadhaa za kisheria. Haki hizi haziko wazi lakini zinafaa kwa mujibu wa sheria. Kwa mfano, pande zote katika mgogoro zinaweza kufungwa na makubaliano ya kutoa uamuzi na si upande wowote utakaojihusisha na mgomo au kuwazuia hadi hatua hiyo iwe imekamilika.

Kwa upande wa bara, migogoro inadhibitiwa chini ya sheria ya 2004 na kutatuliwa kwa usuluhishi kupitia Tume ya Usuluhishi na Upatanishi. Endapo msuluhishi anashindwa kutatua mgogoro ndani ya siku thelathini za rufaa, au kipindi chochote kirefu kilichokubaliwa kwa maandishi na pande zote mbili, upande wowote wenye mgogoro unaweza kutoa notisi ya kusudi lake la kuanza mgomo au kuzuia wafanyakazi waiingie kazini. Kama mgogoro ni wa malalamiko na msuluhishi anashindwa kutatua malalamiko, Tume ya usuluhishi na upatanishi inaweza kumteua msuluhishi kuamua mgogoro, au unaweza kupelekwa kwenye Mahakama ya Kazi.

Mgomo halali au kuzuia wafanyakazi wasiingie kazini kunalindwa chini ya sheria na hakusababishi uvunjaji wa mkataba, wala hakuwezi kuchukuliwa kama kosa la jinai. Mwajiri anaweza kutosimamisha ajira ya mfanyakazi kwa kushiriki katika mgomo halali, au kumfukuza kazi mfanyakazi ambaye anakubali masharti ya mwajiri wakati wa kuzuiwa asiingie kazini. Hakuna mashtaka ya madai au jinai yanayoweza kufunguliwa dhidi ya watu kwa kushiriki katika mgomo halali au kuzuia wafanyakazi wasiingie kazini.

Licha ya lugha ya sheria ya kazi, baadhi ya waangalizi wa haki za kazi, kama vile Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, walitoa malalamiko kwamba Sheria ya 2004 katika

utendaji inaweza kufanya kugoma kuwe kugumu zaidi kwa wafanyakazi katika baadhi ya sekta. Sheria inazuia haki ya kugoma kama kufanya hivyo kungehatarisha maisha na afya ya watu, upungufu ambao unaongezwa na takriban asilimia 50 ya idadi ya wafanyakazi ambao walichukuliwa kama "muhimu" na hivyo, kutoruhusiwa kugoma. Wafanyakazi katika baadhi ya Sekta (maji na usafi, umeme, huduma za afya) na huduma zinazohusiana na maabara, zimamoto na uokoaji, waongoza ndege, mawasiliano ya anga na huduma zozote za usafiri zinazotakiwa kwa utoaji wa huduma hizi) wanazuiwa kugoma na wafanyakazi katika sekta nyingine pia wanaweza kuhusishwa na kukatazwa huko, ama kwa muda au wakati wote, baada ya hatua inayohusisha uchunguzi, notisi, uwasilishaji, kesi ya hadhara na uenezi.

Kwa upande wa bara kuna Kanda Maalumu 23 za Biashara (EPZ), kati ya hizo saba ni waendelezaji wenye leseni na zilizobaki ni waendeshaji wenye leseni. Huko Zanzibar kuna Kanda Huru za Kiuchumi na Kanda pekee za Kiuchumi. Ulinzi wa Sheria ya Kazi unatumika kwa wafanyakazi wa EPZ.

### c. Ukatazaji wa Kazi ya Kulazimishwa au ya Lazima

Sheria inakataza kazi ya kulazimishwa au ya lazima; hata hivyo, kumeendelea kuwepo ripoti mbalimbali kwamba kazi ya kulazimishwa na ya lazima inafanyika kwa watoto na kwamba walikuwa wakisafirishwa kwa ajili ya unyonyaji wa biashara ya ngono.

Sheria inaruhusu wafungwa kufanya kazi bila ya malipo katika miradi kama vile kilimo ndani ya magereza ili magereza yaweze kujitosheleza. Pia wafungwa walitumiwa kama wafanyakazi wa kulazimishwa katika miradi ya nje ya magereza, kama vile ukarabati wa barabara na miradi ya ujenzi ya serikali.

### d. Ukatazaji Ajira ya Watoto na Kiwango cha chini cha Umri wa Kuajiriwa

Ajira ya watoto bado ni tatizo, likiongezwa na VVU/UKIMWI. Takwimu zilizopo za hivi karibuni, kuanzia 2000-01, zinaonyesha kuwa asilimia 35.4 ya watoto wenye miaka mitano hadi 14 walikuwa wanafanya kazi. Sheria inakataza unyonyaji wa watoto mahali pa kazi na inakataza kazi ya kulazimishwa au ya lazima. Utekelezaji kanuni na uanzishaji umekuwa ukitumika, lakini hapakuwa na maendeleo ya kutosha katika utekelezaji wa masharti ya ajira ya watoto.

Ingawa utekelezaji ulikuwa bado duni, serikali ilitekeleza baadhi ya hatua kupunguza tatizo, ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya wakaguzi wa kazi, kuhakikisha kuwa watoto wenye umri wa kwenda shule wanaenda shule, kuweka adhabu kwa wazazi ambao hawaandikishi shule watoto wao, na kuwaelimisha waajiri katika sekta rasmi kutowaajiri watoto wenye miaka chini ya kumi na nane.

Sheria imeweka umri wa chini kwa ajira ya mkataba kuwa miaka 14 na kueleza kuwa watoto wanaweza kuajiriwa kufanya kazi nyepesi tu ambazo haziwezi kuleta madhara kwa afya na ukuaji wao, na haziathiri mahudhurio yao shuleni. Sheria inaeleza kuwa, watoto chini ya miaka 18 hawatakuwa wafanyakazi katika meli au kuajiriwa katika machimbo, kiwanda au eneo lingine lolote la kufanyia kazi ambako mazingira ya kufanya kazi yanaweza kuwa ya hatari, ikiwa ni pamoja na maeneo yasiyo rasmi na kilimo.

Sheria imeweka adhabu za makosa kwa wanaoajiri watoto pamoja na ajira ya kulazimisha; wanaokiuka wanaweza kutozwa faini ya kiasi kisichozidi dola 3,900 (shilingi milioni 5), kifungo cha mwaka mmoja au vyote viwili. Katika mwaka hakuna adhabu iliyotolewa.

Mwaka 2005 Shirika la Kazi Duniani (ILO) na UNICEF waliripoti kwamba watoto wanaoondoka nyumbani kwenda kufanya kazi za ndani katika miji mingine au vijiji, mara nyingi waliishia katika unyonyaji wa biashara ya ngono. Kwa mujibu wa chama cha wafanyakazi wa Mahoteli na Majumbani na ILO, watoto wengi wa kazi za majumbani ni wasichana, wengi wao ni kati ya miaka 13 na 15. Wengi wao wanafanya kazi saa 12 hadi 14 kwa siku, siku saba za wiki bila ya kupumzika au kupata malipo ya ziada kwa kufanyakazi kwa saa nyingi; wakati mwingine wanafanya kazi katika mazingira ya kunyanyaswa.

ILO ilisaidia mradi uliolenga kuongeza kasi ya kuwaondoa watoto katika aina mbaya sana ya ajira ya watoto. Sekta zilizohusishwa zilijumuisha kilimo cha biashara, uchimbaji madini, uvuvi na kazi za ndani. Hadi mwisho wa mwaka jumla ya watoto 4,000 walikuwa wamezuiwa na kuondolewa.

Ajira ya watoto ilisambaa sana Zanzibar; watoto walitumika katika uvuvi, kuchuma karafuu, kazi za majumbani, biashara ndogondogo kama vile kuuza keki, na unyonyaji wa biashara ya ngono karibu na vivutio vya watalii.

Wizara ya Kazi iliendelea kuwajibika kwa utekelezaji wa sheria za kazi kwa pamoja na Tume ya Usuluhishi na Upatanishi na Mahakama ya Kazi. Wizara ilikabiliwa na changamoto ya kiasi kikubwa cha maofisa wake wa kazi katika mwaka. Wizara iliendelea kuendesha semina kuhusu ajira ya watoto katika maeneo mbalimbali nchini.

Kamati za kuratibu ajira ya watoto ngazi ya wilaya na jumuiya na kamati ndogo zilibainisha na kufuatilia kesi za ajira ya watoto, pamoja na viwango tofauti vya ufanisi. Wawakilishi wa ILO, UNICEF na AZISE za nchini zilihitimisha kwamba matatizo haya yalitokana na ukosefu wa fedha na si ukosefu wa utashi wa kisiasa wa kupambana na ajira ya watoto.

Wizara kadhaa za serikali, ikiwa ni pamoja na Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo zina vitengo maalumu vya ajira ya watoto.

Mwezi Oktoba, serikali ilitangaza kima cha chini kipya cha mshahara kuanza kutumika kuanzia Januari 2008. Kuna makundi yanayohusu sekta nane za ajira, pamoja na kiwango cha chini kabisa cha dola 55 (shilingi 65,000) kwa mwezi kwa wafanyakazi wa hoteli na kiwango cha juu kiasi cha dola 300 (shilingi 350,000) kwa mwezi kwa sekta ya madini.

Hata baada ya kuongezewa marupurupu mbalimbali kama vile posho ya nyumba, usafiri, chakula, kiwango cha chini hakikutoa kiwango kizuri cha maisha kwa mfanyakazi na familia, na wafanyakazi walitegemea ukoo wao au kazi ya pili au ya tatu. Katika mwaka, Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, John Chiligati aligundua kuwa baadhi ya wafanyakazi wanafanya kazi saa za ziada bila ya malipo yoyote, kukosa vifaa vya kazi;

na kukosekana kwa fidia ya lazima katika tukio la ajali kazini. Aidha, kwa mujibu wa Waziri, waajiri wengi wa sekta binafsi hawajawaandikisha wafanyakazi wao katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii.

Kulikuwa na ripoti kwamba ili kuepuka masharti ya sheria ambayo yanatoa marupurupu kadhaa na viwango vya chini vya mshahara kwa wafanyakazi walioajiriwa kwa zaidi ya miezi mitatu, waajiri waliwafukuza wafanyakazi kabla ya kipindi cha miezi mitatu kuisha.

Hakukuwa na kiwango cha kisheria cha kazi kwa wiki kwa wafanyakazi wa sekta binafsi, lakini waajiri wengi binafsi walibakia na siku sita, saa 44 – 48 za kazi kwa wiki. Siku tano, saa 40 za kazi kwa wiki zilitumika kwa wafanyakazi wa serikali. Kwa jumla ilikuwa kinyume cha sheria kuajiri wanawake kufanyakazi kuanzia saa 4 usiku hadi 12 asubuhi; hata hivyo, mara nyingi waajiri walipuuza sharti hili.

Sheria kadhaa zinadhibiti usalama mahali pa kazi. Wizara ya Kazi, Ajira, Maendeleo ya Vijana ilisimamia timu ya uchunguzi; hata hivyo, ufanisi wake ulikuwa mdogo. Viwango vya kazi havikutekelezwa katika sekta isiyo rasmi ambako asilimia kubwa ya nguvu kazi ilikuwa imeajiriwa.

Wafanyakazi wangeweza kumshtaki mwajiri kama mazingira yao ya kufanyia kazi hayakulingana na viwango vya afya na mazingira vya Wizara ya Kazi. Migogoro inasuluhishwa kupitia usuluhishi au upatanishi unaofanywa na Tume ya Usuluhishi na Upatanishi.